**Jumatano Septemba 9, 2020** • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580333

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Membe ataja sababu ya kutokurejea CCM

UKURASA 4


Wafanyabiashara EAC sasa waitaka Congo A/Mashariki

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

P W BOTHA

Kwa sheria hizi rushwa uchaguzi inatoka wapi?

UKURASA 11

# WAMEREJESHWA

## NEC yawarudisha wagombea ubunge 15 walioenguliwa, wateule 25 waliokatiwa rufani wapeta... *Endelea uk. 2*

## JPM: Msiuze chakula, njaa inakuja

## TMA yatahadharisha ukame Zanzibar, mikoa 11 Bara

*Endelea ukurasa wa 2*



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage

## YALIYOMO

**UKURASA WA 8**

**SABABU MFUMUKO WA BEI KUBAKI 3.3%**

MFUMUKO wa bei wa Taifa, kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti 2020...

**UKURASA WA 9**

**ASKOFU ATAKA WAUMINI MIKUTANO YA KAMPENI**

KANISA la Anglikana Dayosisi ya Mara, limewataka waumini wake na wananchi wote kujitokeza kwa wingi katika mikutano...

**UKURASA WA 19**

**MADAI YA WATUMISHI KURATIBIWA KIMTANDAO**

SERIKALI imeanza kuratibu madai na madeni ya watumishi yasiyo ya mishahara kwa njia ya kielektroniki...

## MGOMBEA URAIS AOMBA WANANCHI WAMCHANGIE SHILINGI 100

UKURASA 4

**MICHEZO** SIMBA KUIKABILI MTIBWA KIVINGINE UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

Fursa kwa Wagombea! 2020

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# NEC yawarejesha walioenguliwa

**Na Augusta Njoji**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imeanza kutoa uamuzi wa rufani zilizowasilishwa kwake na wagombea wa ubunge walioenguliwa na wasimamizi wa uchaguzi na waliowekewa mapingamizi baada ya kuteuliwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, kati ya rufani 55 zilizopitiwa, 15 zimekubaliwa na wagombea wamerejeshwa kwenye orodha ya wagombea.

Vievile, tume imekataa rufani 15 za wagombea ambao hawakuteuliwa na rufani 25 za kupinga walioteuliwa zimetupwa.

"Tume imechambua vielelezo, nyaraka na maelezo ya warufani na warufaniwa vilivyowasilishwa ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Uchaguzi,"alisema mkurugenzi huyo katika taarifa yake ya jana.

Alisema uamuzi uliofanywa na tume katika rufani hizo umewarejesha baadhi ya warufani kwenye orodha ya wagombea. Dk. Charles alisema tume inaendelea na kazi ya kupitia, kuchambua na kutolea uamuzi rufani za wagombea ubunge zilizowasilishwa na wagombea kupitia kwa wasimamizi mbalimbali wa uchaguzi nchini.

"Kifungu cha 40(6) cha Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343, kinatoa fursa kwa wagombea wa ubunge kukata rufani wanapokuwa hawajaridhika na uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi kutokana na pingamizi zilizowasilishwa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kazi ya kuzijadili na kutolea uamuzi ilianza jana na tume itakuwa inatoa uamuzi na kuwajulisha wahusika kwa kadri rufani hizo zitakavyokuwa zimeshughulikiwa.

Hata hivyo, majina ya waliofanikiwa kurejeshwa na waliokwama katika rufani hizo hayakuwekwa wazi kwa umma, mkurugenzi huyo alisema tume inaendelea kutoa matokeo baada ya usajili na uchambuzi wa rufani hizo kuanzia jana na kwamba wahusika watajulishwa kwa barua.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, akizungumza na Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Donald Wright, alipotembelea ofisini kwa waziri, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JPM: Msiuze chakula, njaa inakuja

**Na Gwamaka Alipipi, SENGEREMA**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli, amewataka Watanzania kutoingia tamaa ya kuuza mazao, bali wayatunze kwa mahitaji ya baadaye.

Amesema hivi sasa kuna wafanyabiashara wanazunguka vijijini wakitaka kununua mazao, hivyo amewataka kutoingia tamaa ya kuuza haraka kwa sababu mataifa mengi hayakuzalisha chakula wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Magufuli alisema hayo jana wilayani hapa, wakati akiwahutubia wananchi na wanachama wa CCM katika mkutano wa kampeni, waliojitokeza kumsikiliza katika viwanja vya mnadani akiomba kura.

"Tumepata mazao mengi, tusiyauze haraka haraka tutapata njaa. Mkitaka kuyauza uzeni kwa bei ya juu, watu sasa wanazunguka kutafuta chakula kwa sababu hawakulima wakati wa mlipuko wa corona. Wanatafuta mchele, mahindi, maharage," alisema Magufuli na kuongeza:

"Sengerema ni wakulima wazuri, ninawaomba mazao msiyauze. Dunia imekumbwa na corona, wakati ugonjwa huo unaanza nchi nyingi zilifungia watu wake ndani, sasa watu wote ambao walifungiwa kwenye nchi hizo hawakufanya chochote, wana njaa, nchi inayotegemewa ni Tanzania."

Rais Magufuli alisema wakati wa mlipuko wa ugonjwa huo, Tanzania ilimwomba Mungu ugonjwa huo uondoke, hivyo hakukuwapo na Mtanzania aliyefungiwa ndani.

Aidha, aliwaambia wananchi wa Sengerema faida zinazopatikana kutokana na ujenzi wa daraja la Kigongo-Busisi lenye urefu wa kilometa 3.2, linalojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 700.

Rais Magufuli alisema wananchi wa Sengerema watapata ajira pamoja na kujipatia fedha pindi ujenzi wa daraja hilo utakapoanza.

Pia aliwataka vijana, mama lishe, wafanyabiashara wadogo kutoka Sengerema kuchangamkia fursa zitakazopatikana kwenye ujenzi wa daraja hilo.

"Tunajenga daraja kwa fedha zetu, hatujakopa kwa mtu yeyote, fedha zitakazotumika kujenga daraja hili tumezitoa kwa mafisadi, tuliwabana. Ni daraja refu Afrika Mashariki. Fedha ambazo zimetolewa si kidogo, hakuna aliyetegemea tungejenga daraja hilo, ujenzi wa awali umeshaanza," alisema.

"Ndiyo maana nimekuja kuwaomba kura wana Sengerema, mradi kama huo wa Sh. bilioni 700 akiletwa mtu mwingine atanyofoa machuma na kwenda kuuza, ndugu zangu uongozi haujaribiwi, ziko nchi ambazo zilijaribu na matokeo mmeyaona," aliongeza.

Kuhusu mafanikio yaliyopatikana wilayani Sengerema kwa miaka mitano, Magufuli alisema serikali imejenga madarasa 167, ukarabati wa miundombinu ya shule za sekondari kwa gharama ya Sh. bilioni 1.03.

Alisema pia kumejengwa hospitali mbili za katika Wilaya ya Buchosa na Sengerema kwa gharama ya Sh. bilioni 3.2. ujenzi wa vituo vya afya vitatu.

# Serikali yatangaza tishio la ukame

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imesema kuna uwezekano wa baadhi ya mikoa kukumbwa na ukame na kuwashauri wakulima kulima mazao yanayostahimili hali hiyo.

Imeelezwa kuwa uwezekano wa kutokea ukame unatokana na upungufu mkubwa wa mvua unaotarajiwa kutokea katika kipindi cha mvua za vuli nchini.

Hayo yalibainishwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), na kubainisha kuwa katika kipindi cha mvua za Oktoba, Novemba na Desemba mikoa mingi itakuwa na upungufu mkubwa wa mvua.

TMA ilitoa tahadhari hiyo jana wakati wa utabiri wa mvua hizo zinazotarajiwa kuanza wiki ya pili ya mwezi huu katika mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka na zinatarajiwa kufika kikomo Januari mwakani.

Akizungumza na waandishi wa habari , Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, alisema mifumo ya hali ya hewa inaonyesha kutakuwa na mvua ndogo kufika chini ya wastani kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Zanzibar, baadhi ya maeneo ya mkoa wa Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Mara na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Kigoma.

"Hali hii inatokana na joto la bahari katika eneo la kitropiki ya Bahari ya Pasifiki iliyoko chini ya wastani na inatarajiwa kuendelea kuwa hivyo katika kipindi chote cha msimu wa Oktoba mpaka Desemba, hali hii inatarajia kupunguza nguvu ya mifumo inayosababisha mvua katika maeneo mengi yaliyotajwa," alisema Dk. Kijazi.

Alisema hali hii itapelekea kutokea kwa athari mbalimbali zitakazotokana na hali ya ukame kwa maeneo yatakayokosa mvua.

"Kwenye sekta ya kilimo na usalama wa chakula, tunategemea upungufu wa unyevunyevu katika udongo na hivyo kufanya kilimo kutostawi na ndio maana tunashauri kilimo cha mazao yanayostahimili ukame, lakini tunategemea visumbufu vya mazao na magonjwa vinatarajiwa kuongezeka hivyo hatua za tahadhari zinahitajika," alisema Dk. Kijazi.

MAGONJWA YA MIFUGO KUPUNGUA

Aidha, alisema kutakuwa na hali ya kupungua kwa magonjwa ya mifugo na mazao ya uvuvi kama samaki na mwani, pia kutakuwa na mtiririko mfupi wa maji na kuathiri malisho ya mifugo.

"Hali hii naweza ikasababisha migogoro kati ya wafugaji na wakulima, hivyo mamlaka husika sasa iangalie njia bora ya kukabiliana na hali hii itakapojitokeza," alisema.

Hata hivyo, ukosefu wa mvua utafaidisha sekta ya usafiri wa anga na nchi kavu. Kadhalika, TMA imeshauri mamlaka husika kutumia kipindi hiki kwa ajili ya kuimarisha ujenzi wa miundombinu hususani sehemu korofi zinazoathiriwa na mafuriko.

Aidha, kwa upande wa sekta ya nishati, maji na madini, inatarajiwa kuwapo kwa upungufu wa maji katika mabwawa, hivyo TMA inashauri maandalizi ya nishati mbadala za umeme ili kukabiliana na upungufu endapo utatokea.

SERIKALI YAJIPANGA


Msemaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, Ibrahimu Hamidu, alisema:

"Kinachotokea ofisi ya Waziri Mkuu huwa inatoa maelekezo kwa kamati husika pale panapotokea maafa, hivyo kujua ni namna gani mikoa imejipanga, hilo ni jukumu la ma Ras katika mikoa husika."

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustine Kamuzora, alisema:

"Hatujapata hiyo taarifa, lakini baada ya kuipata lazima tuchukue hatua kwa kuitisha kikao cha kamati na kujadiliana."

TANGAZO


NMB
Karibu yako
NMB Mastercard Prepaid Card
Kwasababu unaweza kutengeneza kumbukumbu
NMB prepaid
1234 5678 9012 3456
#ulimwenguusionakikomo
Kwa Malipo Dunia Nzima
ATM, Mashine za Malipo na Malipo ya Mtandaoni
Furahia Nyakati
Kwa taarifa zaidi piga 0800 002 002
Vigezo na Masharti kuzingatiwa.
www.nmbbank.co.tz

# Membe ataja sababu ya kutokurejea CCM

**Thobias Mwanakatwe, DODOMA**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Bernard Membe, amesema hawezi kuondoka katika chama hicho na kurejea Chama Cha Mapinduzi (CCM) baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Ametaja sababu kubwa kwake kutorejea CCM kuwa ni kutokana na chama hicho kumfukuza na siyo kujitoa kwa hiari yake mwenyewe kama ilivyokuwa kwa wanachama wengine waliojitoa na baadaye kurejea kwenye chama hicho.

Vilevile, Membe amesema upinzani siyo kupinga kila jambo linalofanywa na serikali inayokuwa madarakani.

Waziri huyo wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, aliyasema hayo juzi wakati akihojiwa katika kipindi cha 'Dakika 45' kinachorushwa na kituo cha runinga cha ITV.

Akijibu swali aliloulizwa kuhusu hofu ya Watanzania kumchagua na baada ya Oktoba kurejea tena CCM, Membe alisema kamwe hawezi kurejea CCM kwa sababu alifukuzwa, akisisitiza kuwa wanaoondoka na kisha kurejea katika chama ni wale ambao walijitoa wenyewe.

"Kila ninapopita wananchi wanaonyesha mabango wakisema Membe, Membe sasa unachaguliwa kuwa rais unaondokaje, nitakuwa nimevunja katiba.

"Ona Maalim Seif alifukuzwa, sijamwona akirudi. Zitto Kabwe alifukuzwa kwenye chama chake. Sijamwona akirudi. Waliofukuzwa ni vigumu kurudi kwa sababu wamefungiwa milango, halafu hata ukirudi, wewe mwenyewe utajidhalilisha," alisema.

Membe alisema kuwa baada ya kufukuzwa CCM, alikaa chini kuchagua chama cha kwenda na akachagua ACT-Wazalendo chenye mshikamano na vijana wenye ari ya kutaka mabadiliko katika nchi bila uoga.

"Chama chochote kinachoingia kwenye matatizo, ACT inakuwa mstari wa kwanza kupinga jambo lile kwa sababu chama hicho kinapenda mabadiliko, uwazi na kusaidia kuwasemea walio wengi," alisema.

Kuhusu vyama vya upinzani, alisema upinzani huwezi kukosoa kila kitu na ni lazima ukubali kuna mambo yanafanyika vizuri, japo wapo baadhi ya wanasiasa ambao alidai wanaona upinzani ni kama uadui wakati siyo kweli.

Akizungumzia kuhusu kuitaja CCM mara kadhaa anapokuwa katika shughuli za ACT-Wazalendo, Membe alisema siyo dhambi na hilo linaonyesha ametoka katika chama ambacho kimemkuza na kumpanua.

"Ukiona mtu hakosei, ujue huyo hakuzama kwenye siasa ya kweli huko alikotoka. Ni lazima ukosee kwa sababu nimekuwa mwanachama wa CCM kwa muda wa miaka 35. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile lazima nikosee," alisema.

Membe aliongeza kuwa kuondoka kwenye CCM na kwenda kujiunga kwingine hakuna maana anadharau chama kingine. Alipoulizwa kuhusu sababu za kuwania urais, Membe alisema ni kwa sababu anatekeleza matakwa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ambayo yanaangalia nani anafaa kuwa rais na kwamba ana uzoefu uliojikita katika maendeleo ya wananchi kulinganisha na wagombea wenzake.

"Ningefanya dhambi kubwa sana kama nisingegombea, sitaki wananchi waje waniambie wewe Membe ungegombea tusingefikishwa hapa. Ninataka niwaambie 'niliwaomba mkaniyima wenyewe'," alisema.

Membe alijiunga na ACT-Wazalendo Julai 15 mwaka huu, baada ya kufukuzwa uanachama CCM kutokana na tuhuma za kukiuka maadili ya chama hicho kinachoongoza serikali.

## Mgombea wa urais aomba kila mwananchi amchangie 100/-

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), Profesa Ibrahim Lipumba, amesema vyama vya upinzani vinakabiliwa na hali ngumu kiuchumi na vinafanya kampeni kwa shida.

Akihojiwa katika kipindi cha 'Dakika 45' cha ITV kilichorushwa usiku wa kuamkia leo, Profesa Lipumba alisema vyama vinaomba michango kutoka kwa wanachama na wananchi wengine ili kufanya kampeni nchi nzima.

Alisema inabidi kutafuta misaada kutoka kwa wanachama ili kusaidia kufanya kampeni na kwamba chama chake kinaomba Watanzania kukichangia walau Sh. 100 kwa kila mwananchi.

"Kwanza, hali ya uchumi ya Watanzania kwa ujumla ni mbaya, hali ya fedha, agenda ya vyuma vimekaza ni kweli, wafanyabiashara wamekuwa na wasiwasi kwamba wakifanya hivyo (kutoa mchango kwa vyama vya upinzani) inaweza kuwaletea matatizo," alisema.

"Tunarudi kwa Watanzania kutaka kuleta mabadiliko, tunahitaji kuleta mabadiliko kwa sababu hali ya maisha ni ngumu, tumetoa wito kila Mtanzania ajiwekee Sh.100 kwa siku 50 hadi 60 watatuchangia Sh. 6,000.

"Ikiwa nusu milioni watatuchangia, tupata jumla Sh. bilioni tatu, zitatutosha kufanya kampeni nchi nzima. Hata akiwa na hali ya maisha ngumu, akituchangia Sh. 100 haiwezi kuongeza ugumu wa maisha alionao.

"Kuna wafanyabiashara watuchangie, kwa kuwa chama chetu kinaandaa mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji, alipe kodi kwa amani na mazingira mazuri ya biashara," aliomba.

Profesa Lipumba pia alisema anawania urais kwa kuwa Tanzania ina rasilimali, lugha ya Kiswahili inaunganisha wananchi na hakuna matatizo ya udini na ukabila.

"Tunapaswa kuwa taifa lililopiga hatua, lakini la kusikitisha hadi sasa Watanzania walio wengi ni maskini wa kutupwa. CUF sera yetu ya msingi ni haki sawa na furaha kwa wote," alitamba.

Alipoulizwa kuhusu hoja ya kuwa yeye siyo mpinzani halisi, Profesa Lipumba alitamba kuwa yeye ndiye mpinzani pekee anayeihoji serikali bila woga, huku akitaka wananchi kupuuza propaganda zilizopo dhidi yake.

Alisema CUF ikishika madaraka ya kuongoza nchi, itawekeza kwenye kilimo ili kuleta mapinduzi ya viwanda ambavyo vitatoa ajira kwa wananchi wengi.

"Katika kila Sh. 100 iliyotumia na serikali fedha iliyokwenda kwenye kilimo ni Sh. tatu, huwezi kuleta mapinduzi ya kilimo kama huwekezi kwenye kilimo. Sisi tutaleta mabadiliko," alitamba.

"Kaulimbiu yetu ni haki sawa na fursa kwa wote. Nikichaguliwa kuwa rais, nitaunda serikali ya umoja wa kitaifa ili kukamilisha katiba ya demokrasia yenye misingi ya kweli ambayo itakuwa dira ya nchi.

Profesa Lipumba alisema serikali ya umoja wa kitaifa wanayokusudia kuiunda, itasimamia haki za kisiasa, kiuchumi na kijamii, mambo yanayokwenda sambamba na Malengo Endelevu ya Milenia (SDGs).



Mkuu wa Mkoa mstaafu, Aggrey Mwanri (kulia), akimnadi mgombea ubunge wa Jimbo la Siha (CCM), Dk. Godwin Mollel, katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu uliohutubiwa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (hayupo pichani) katika kijiji cha Matado wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro jana. **PICHA: OWM**

## Majaliwa: JPM chaguo sahihi

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Watanzania wana kila sababu ya kumchagua Rais John Magufuli katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Amesema sababu kubwa ni kiongozi makini, shupavu, mbunifu na mwenye uwezo wa kusimamia vizuri rasilimali za taifa kwa manufaa ya wananchi wote.

Majaliwa alisema hayo jana alipokuwa akimwombea kura Rais Magufuli, mgombea ubunge wa Jimbo la Siha, Dk. Godwin Mollel na wagombea udiwani kwa tiketi ya CCM kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika katika kijiji cha Matadi, kata ya Ndemet Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano ya awamu ya kwanza ya uongozi wake, Rais Magufuli amefanya mambo mengi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini na yamewanufaisha Watanzania wote wakiwamo wakazi wa Wilaya ya Siha bila ubaguzi wowote.

Watanzania, alisema wanatakiwa wamchague Rais Magufuli ili awaongoze katika kusimamia vizuri matumizi ya rasilimali za taifa kwa ajili ya maendeleo na kuendelea kudumisha amani na utulivu uliopo nchini.

Majaliwa alisema Tanzania ni nchi tajiri yenye uwezo wa kuwaletea wananchi wake maendeleo bila utegemezi, hivyo wachague viongozi makini kwa manufaa ya taifa.


"Wana Siha wote nimekuja hapa kwenu leo (jana) nina kazi moja tu ya kumwombea kura mgombea wa nafasi ya urais kupitia CCM, Rais Dk. Magufuli ambaye ni kiongozi imara, mzalendo na mchapakazi, mgombea ubunge wa Jimbo la Siha Dk. Mollel na wagombea udiwani wote wa CCM katika wilaya hii. Ikifika siku ya kupiga kura tuhakikishe tunawachagua," alisema.

Majaliwa alisema lazima wananchi waamini kwamba uongozi unatoka kwa Mwenyezi Mungu na Rais Dk. Magufuli ameletwa na Mwenyezi Mungu, hivyo akawaomba wampe ridhaa ya kuongoza katika miaka mitano mingine, ili aendeleze kazi za maendeleo alizozianza.

Majaliwa ametumia fursa hiyo kuwahakikishia wananchi wa Siha kuwa serikali itayarudisha mashamba yote ya Chama Kikuu cha Ushirika cha Kilimanjaro (KNCU) yanayomilikiwa kinyemela na watu wachache kwa manufaa yao binafsi.

Alisema KNCU ni mali ya wananchi (wana ushirika) na kwamba serikali imefanya kazi kubwa ya kurudisha hadhi ya ushirika katika kipindi cha miaka mitano, ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani waliohusika kufanya ubadhirifu katika vyama hivyo na itaendelea kurejesha mali zote kwa wananchi ili wafanyie shughuli za maendeleo.

TANGAZO


CHUKUA
KILICHO
CHAKO
Usipoteze kilichobakia
kwenye bando yako ya awali!
24h
Kifurushi cha Siku
Beba kilicho salia kwenye bando yako
ya awali, kwa kununua bando ile ile
kabla muda wake haujaisha.
4G+
Piga *147*00#
chagua Siku, Wiki au Mwezi.
Kwa vigezo na masharti tembelea: www.tigo.co.tz
tigo

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wenye ulemavu wamesahaulika uchaguzi 2020

KAMPENI za uchaguzi zinazidi kushika kasi kwa wagombea wa nafasi ya urais, ubunge na udiwani kuzunguka maeneo mbalimbali kuomba ridhaa ya kuongoza kwa miaka mitano.

Tayari makundi mengi yamefikiwa hasa yale yasiyo na changamoto zozote za viungo, ila kundi la watu wenye ulemavu wa kusikia wanahitaji lugha ya alama na wasioona ambao anahitaji maandishi nundu wameachwa kando na wasioweza kutembea.

Katika mchakato wa uchaguzi kila chama kinajitajidi kuwafikia wapigakura kwa kila namna ikiwa ni kupitia mikutano ya hadhara ambayo wananchi kufika wenyewe kusikiliza sera, kuwatembelea, mitandao ya kijamii na machapisho mbalimbali.

Kundi la wenye ulemavu wa aina mbalimbali ni vigumu sana kupata taarifa sahihi kutoka kwa wagombea na ndiyo maana wakati wa mchakato wa maandalizi ya uchaguzi wanakuwa wakisikika wakiiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuhakikisha vyama vinawakumbuka na uwekwe utaratibu wa kundi hilo kupiga kura wenyewe bila kusaidiwa.

Kutokana na changamoto zilizopo, kuna uwezekano kundi la watu wenye ulemavu likaachwa nyuma wakati wa uandikishaji na majina yao kutokuwapo katika daftari la mpigakura na kukosa kitambulisho cha mpigakura.

Mathalani, kundi hilo halijafikiwa ipasavyo na vyombo vya habari kutokana na changamoto walizonazo, hivyo kuachwa nyuma, kwa mfano wasiosikia walitarajia kuwa na wakalimani katika kila kampeni ili waweze kuelewa kinachozungumzwa na kufanya maamuzi kwa akili zao wenyewe.

Tangu kuanza kwa kampeni hizo si kwenye vyombo vya habari, mikutano ya kisiasa hatujaona kukiwapo wakalimani au ilani za vyama kutengenezwa kwa nukta nundu, ili kuwawezesha wenye ulemavu wa kuona na kusikia kujua kilichopo ambacho ni ahadi kwa miaka mitano ijayo.

Mara kwa mara NEC imesisitiza kuvitaka vyama kuhakikisha kundi la wenye ulemavu linashiriki kikamilifu, lakini bado halijapata nafasi ifaayo kwa ajili ya kupiga kura au kujiandikisha.

Ili uchaguzi uwe shirikishi, ni lazima wananchi wote wapate nafasi ya kupiga kura ya siri ndani ya sanduku la kura, kuwe na miundombinu rafiki kwa makundi yote na ikiwezekana kutenga eneo kwa ajili yao kutimiza wajibu wao wa kikatiba.

Tunavihimiza vyama vya siasa kuangalia suala hili kwa jicho la pekee au vyombo vya habari vya umma kuhakikisha wakalimani wanakuwapo kwenye runinga wakitafsiri kwa alama, ili waelewe ahadi zinazotolewa kuliko baadaye kuhadithiwa.

Tukumbuke watu hawa ni kutoka ndani ya familia zetu, kuwapoteza wao ni sawa na kupoteza kura nyingi ambazo zinaweza kuwa nguzo ya ushindi, bado zinahitajika jitihada za vyama kuonyesha wamewafikia kwa njia mbalimbali.

Unapoacha nyuma kundi moja katika suala la maendeleo maana yake mambo yao watasemewa na kundi jingine ambalo kwa namna moja au nyingine haliwezi kuvaa viatu vyao na vikawaenea.


Wajibu huo haushii kwa vyama pekee, bali mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyopewa jukumu la kutoa elimu ya mpigakura kwenye uchaguzi mkuu, kuhakikisha elimu inayafikia makundi yote, atumie mbinu mbalimbali.

Inatarajiwa mashirika hayo kwenda maeneo ya vijijini na kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji kama vipeperushi na maandiko mbalimbali kuwafikia wapigakura.

Maamuzi ya kupiga kura yanategemea mambo mengi ikiwamo mtu kuona umuhimu wa kushirikia kupiga kura na thamani ya kura yake, ushawishi wa vyama. Hata hivyo, haitarajiwi kwa namna yoyote kuwa na ulaghai kwa kutumia mali, fedha au ahadi za vyeo na ajira ili kupata nafasi husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Faustine Feliciane

# Inawezekana kuepuka athari hizi za ukame

WAKATI Watanzania wanaelekeza macho na masikio yao kwenye msimu wa vuli

Mamlaka Hali ya Hewa (TMA), inatoa angalizo kuhusu msimu wa vuli na kuwahimiza wakulima wachukue tahadhari

TMA inatabiri kuwa mikoa ya Mwanza, Geita, Simiyu, Mara na Shinyanga, lakini pia Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Dar es Salaam, Pemba na Unguja, huenda ikakabiliwa na ukame.

Inatoa utabiri wa msimu wa mvua za vuli zinazotarajiwa kuanza wiki ya pili ya Septemba hadi Januari mwakani na kutahadharisha kuwapo ukame

kwa mikoa hiyo inayopata mvua mara mbili kwa mwaka.

Mikoa hiyo imeshuhudia mvua nyingi kwa hivyo kuleta neema lakini pia kusababisha athari mbalimbali zitokanazo na mvua kama mafuriko na uharibifu wa maisha, mazao na mali.

Hayo yamo katika taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Agnes Kijazi.

Katika kuelekea kwenye hali hiyo ya ukame,ni vyema sasa wananchi pamoja na mamlaka za mikoa hiyo zinazosimamia kilimo na mazingira kuchukua tahadhari ya hali hiyo ikiwa ni pamoja na kuhifadhi chakula ambacho kitahitajika zaidi katika kipindi cha ukame.

Kwa mujibu wa Ofisi wa Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, sheria zilizopo sasa zinatoa nafasi kwa Kamati za Maafa za Mikoa zinazoongozwa na Makatibu Tawala wa Mikoa (RAS) kusimamia na kuchukua hatua pale kunapokuwepo na tahadhari ya maafa mathalani ukame unaotarajiwa.

Kwa msingi huo ni vyema kamati hizo

kuanza mapema kufuatilia athari zitakazotokea na kuchukua tahadhari, kujipanga, kukabiliana na kupunguza athari.

Taarifa ya TMA, inaeleza kuwa

athari za ukosefu wa mvua katika kipindi hiki cha mvua za vuli zitaonekana kwenye sekta mbalimbali kama kilimo na ufugaji, uvuvi, nishati, maji na madini.

Aidha, utaathiri usafirishaji, utalii na wanyamapori, mamlaka za miji pamoja na ya afya.

Kwenye sekta ya kilimo, TMA imesisitiza tahadhari kwa wakulima wa mikoa hiyo kuangalia kilimo kitakachohimili ukame.

Katika kilimo pamoja na kuwa mamlaka zinawajibu wa kuwaelimisha na kuwashauri wakulima, mkulima mwenyewe ana jukumu la kuchukua tahadhari kwa kuanza sasa mipango ya kulima mazao yanayohimili ukame .

Pia, kuhifadhi chakula ili kukabiliana na upungufu unaotokana na uhaba wa mvua.

Aidha, kwa upande wa mipango miji, kama ambavyo Mkurugenzi Mkuu wa TMA alivyoelekeza ni vyema sasa kwa yale maeneo ambayo yamekuwa korofi kwenye miundombinu kama barabara hususani wakati wa mvua hatua za kuboresha na kujenga maeneo hayo zifanyike sasa.

Kazi ifanyike wakati ambao hakuna mvua ili kurahisisha ukarabati wake.

Kamati za maafa za mikoa zinazoongozwa na RAS zinapaswa kuanza kuchukua hatua sasa kwa kuweka mipango ya namna ya kukabiliana na hali yoyote itakayotokea kutokana na upungufu huo wa mvua unaoelezwa.

Kamati hizo zisaidiane na wananchi katika maeneo husika kujipanga na athari zitakazotokana na ukame ambao unatokana na mvua kunyesha chini ya wastani kwa maeneo mengi.

Lakini pia Watanzania wafuatilie utabiri wa kila siku zitolewazo na TMA kupitia vyombo vya habari mbalimbali ili kufanya yale yanayoelekezwa na kujiepusha na athari.

Hali hii ya ukame unaotarajiwa kutokea katika mikoa iliyotajwa inaweza isiwe kikwazo kikubwa kwa wananchi katika maisha yao ya kila siku endapo tu tahadhari zitachukuliwa mapema na kila upande kujipanga.

Endapo taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na TMA zikiwafikia wananchi kwa wakati na kufanyiwa kazi, athari za majanga yanayotazamiwa zinaweza kupungua.

## HABARI KITAIFA

# Watumiaji vyombo usafiri waonywa kujaziwa mafuta pampu zisizo bora

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA wameshauriwa kutokubali kuwekewa mafuta kwenye vituo vya mafuta kwa kutumia pampu ambazo hazijawekewa stika za Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA).

Ushauri huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala, Stella Kahwa, wakati wa mafunzo kuhusu vipimo kwa madereva wa pikipiki za abiria, maarufu kama bodaboda.

WMA iko kwenye kampeni endelevu kuelimisha makundi mbalimbali kuhusu vipimo sahihi na namna ya kubaini vile vilivyoghushiwa na jana ilikuwa zamu ya madereva wa bodaboda.

Kwa mujibu wa Kahwa, WMA imehakiki na kuweka alama kwenye vituo vyote vya mafuta nchini hivyo ni vyema mteja akajiridhisha kama stika hiyo ipo kabla ya kuwekewa mafuta.

Alisema wamekuwa wakifanya ukaguzi wa mara kwa mara kuangalia kama kuna wafanyabiashara ambao wanacheza na pampu za mafuta kwa lengo la kuwaibia wateja wao. Baadhi ya bodaboda waliopata mafunzo hayo waliishukuru WMA kwa kuwakumbuka na kuwapa mafunzo ambayo yamewafumbua macho kwani wengi wao walikuwa hawajui vipimo sahihi.

Mmoja wa madereva hao wa bodaboda, Peter Japhet, aliishukuru serikali kupitia WMA kwa kuwakumbuka na kushauri kwamba elimu hiyo inapaswa kuwa endelevu kwa makundi mengine.

"Wengi tuliokuja hapa hatujui vipimo sahihi sasa tumeelimishwa ili tukawaelimishe wengine kwa sababu watu wengi hawajui kwamba kwenye mizani huwa kunakuwaga na wizi," alisema.

Mazina Nichodemus wa Kigogo Fresh, alisema wafanyabiashara wengi wamekuwa wakifanya udanganyifu kwenye vipimo hivyo elimu waliyoipata itawasaidia kuelimisha wengine.

Alisema watu wengi wamekuwa wakinunua bidhaa na kupimiwa bila kuhakiki mizani kama ina stika ya WMA, hivyo kuna umuhimu wa elimu hiyo kuwa endelevu kwenye mikoa yote.

Dereva mwingine, Hussein Omar alisema baadhi ya wenye maduka na wafanyabiashara wamekuwa na kawaida ya kucheza na mizani kwa lengi la kuwaibia wanunuzi.

# Vyuo vikuu vyaunga mkono uchumi wa kati

**Na Romana Mallya**

**"Tunataka vijana wanaomaliza chuo wakifika mtaani wasijibweteke kwa kungoja ajira, wajiajiri kupitia ubunifu walizoibua chuoni, waendeleze yale waliyobuni, siyo tu itakabiliana na changamoto ya ajira, pia itawezesha kuendana na uchumi wa viwanda," alisema.**

VYUO vikuu nchini vimeeleza kuunga mkono azma ya serikali ya uchumi wa kati kwa kuhakikisha wanazalisha wataalamu wa kuanzisha, kuviendeleza na kuvisimamia viwanda kupitia ubunifu unaoibuliwa na wanafunzi vyuoni.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, kuhusu namna ambavyo vyuo vinalinda ubunifu na kuunga mkono uchumi wa kati wa viwanda, wakuu kadhaa wa vyuo hivyo walisema lazima ubunifu wa vijana vyuoni ulindwe na uendelezwe baada ya kumaliza vyuo.

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Prof. Lughano Kusiluka, akizungumza wakati wa maonyesho ya elimu ya juu, sayansi na teknolojia yaliyofungwa Jumamosi, alisema wanapozungumza uchumi wa kati, maana yake ni biashara, utawala sheria, ujasiriamali ambavyo vyote vinafundishwa vyuoni.

"Popote duniani huwezi kuendesha uchumi bila ya kuwa na wataalamu, wajasiriamali, utaalamu wa fedha na kuwa na wanasheria wazuri... kwa hiyo kama vyuo hii ndiyo kazi yetu kuwazalisha ili waunge mkono kazi inayofanywa na serikali yao," alisema.

Prof. Kusiluka alisema chuo hicho kimebobea katika maeneo ya utawala, biashara, uchumi, ujasiriamali na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ambavyo vinaendana na uchumi wa kati wa viwanda.

Naye Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema lazima ubunifu unaofanyika vyuoni ulindwe kwa ajili ya faida ya wanafunzi baadaye.

Alisema pamoja na utoaji wa elimu unaoendelea chuoni hapo kuanzia ngazi ya cheti hadi Shahada ya Uzamili, wamekuwa wakiwajengea uwezo na maarifa wanafunzi ili yawasaidie kuhimili ushindani wa soko la ajira mtaani.

"Tunataka vijana wanaomaliza chuo wakifika mtaani wasijibweteke kwa kungoja ajira, wajiajiri kupitia ubunifu walizoibua chuoni, waendeleze yale waliyobuni, siyo tu itakabiliana na changamoto ya ajira, pia itawezesha kuendana na uchumi wa viwanda," alisema.

Prof. Mwakalila alisema ni lazima vijana wajengewe uwezo tangu wadogo badala ya kutoka chuoni bila kuwa na ubunifu wowote.

"Nchi zilizoendelea mfano China vijana wanajengewa uwezo tangu wadogo na wanafanya mambo makubwa kila siku wanabuni vitu na kuviendeleza," alisema.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## MWITO WA KUTOA MAONI

*Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.*

*Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.*

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Pmax Co. Ltd- Njombe Service Station S.L.P 637 Njombe | Kiwanja Na. 219, Kitalu "T", eneo la Nazareth, Njombe Mjini, Mkoa wa Njombe | Max Kanut Mlelwa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 2. | Njombe Filling Station S.L.P 411 Njombe | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", Kijiji cha Lupembe, Wilaya ya Njombe, Mkoa wa Njombe | James Malika Mwinuka (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 3. | Kapunga Rice Project Limited S.L.P 45 Chimala - Mbeya | Kiwanja Na. 628/2, Kijiji cha Kapunga, Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya | Antoneta Sebastian Fialho (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 4. | SBC Tanzania Limited S.L.P 4162 Dar es salaam | Kiwanja Na. 54-57, Eneo la Kipawa, Wilaya ya Ilala, Dar es salaam | Ziad El Khalil (Raia wa Uingereza) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 5. | Matemba Filling station S.L.P 141 Turiani | Eneo la Sungaji, Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro | Dickson Matemba (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 6. | Ahmed Abdallah Bakhamis S.L.P 20 Kilosa | Kiwanja Na. 1, Kitalu A, Eneo la Kibaoni, Wilaya ya Kilosa, Mkoa wa Morogoro | Ahmed Abdallah Bakhamis (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 7. | Landmark Filling Station Mvumi, Kongwa, Dodoma | Eneo la Mvumi, Kata ya Mvumi, Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma | Fatuma Ramadhan Mganga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 8. | Landmark Filling Station Hombolo, S.L.P 64. Kongwa, Dodoma | Eneo la Hombolo, Kata ya Hombolo, Wilaya ya Dodoma Mjini, Mkoa wa Dodoma | Fatuma Ramadhan Mganga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 9. | Khalid Salum Said T/A Green Apple Filling Station S. L. P 80, Kigoma | Kiwanja Na 6MD, Kitalu A, Eneo la Mlole, Manispaa ya Kigoma-ujiji, Mkoa wa Kigoma | Khalid Salum Said (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

**Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.**

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**



TOTAL
Total Tanzania

## TAARIFA KWA UMMA

## Total Tanzania yazidi kupanua wigo wa biashara zake nchini

Dar es salaam, Septemba 4, 2020- Mnamo tarehe 1 Septemba 2020, Total Tanzania ilizindua kituo chake cha nane (8) chenye mfumo ujulikanao kama DODO (Dealer Own, Dealer Operated) maeneo ya Goba Dar es salaam. Kituo hiki ni sehemu ya mtandao mkubwa wa kampuni ya Total Tanzania LTD wenye zaidi ya vituo 90 nchini.

Kinyume na taarifa zilizosambazwa na ambazo zimekanushwa, Total Tanzania ina mpango wa kimaendeleo wa muda mrefu nchini na kampuni hiyo imekuwa ikifanya biashara kwa zaidi ya miaka 50 Tanzania. Sherehe za ufunguzi wa kituo kipya cha Total Mchigani ni uthibitisho tosha wa kampuni ya Total kujikita kwenye uwekezaji na ukuaji wa biashara zake nchini.

**Kwa Maswali.**
**Media Relation:**
**Marsha Msuya**
**0786 999 746**

**Kuhusu Total Tanzania**
Total Tanzania ni kampuni ya Mafuta ya petroli iliingia nchini Tanzania tangu mwaka1969. Biashara ya Total Tanzania inalenga katika kutoa huduma za usambazaji na uuzaji wa mafuta ya petroli, dizeli vilainishi na bidhaa za mafuta, ambayo ni kuuzwa katika vituo mbalimbali vya mafuta na pia katika idara maalum ndani ya wake shirika hilo. Total Tanzania Limited inatumia utaalamu wake katika kutoa huduma za kuaminika kwa wateja wake kwa mfumo wa kadi maalum " Kadi ya Total" kwa ajili ya ununuzi wa mafuta na huduma mbalimbali magari katika vituo vya mafuta vya Total Katika kujitanua kibiashara kuelekea kwenye matumizi ya nishati mbadala, kampuni ya Total Tanzania Limited kupitia mradi wake wa Total Access to Solar (TATS) project, inasambaza taa za nishati jua zinazoitwa AWANGO kwa jamii ya Watanzania

Pia kampuni ya Total imenunua kampuni ya GAPCO Tanzania pamoja na kiwanda cha kutengeneza vilainishi nchini ili kuzidi kuwafikiwa Watanzania kwa urahisi na kuwapa huduma na bidhaa zenye ubora.
Kuhusu Kampuni ya Total

Total ni kampuni ya kimataifa ya nishati ya mafuta na gesi ni ni moja ya makapini ya kwanza kabisa ya kimataifa kujihusisha katika nishati ya jua duniani kote. Ina wafanyakazi 100 000 wenye kuchangia dhima ya kampuni : kuzalisha nishati bora na safi na salama, na kuizalisha kwa ufanisi zaidi, nguvu zaidi na ubunifu wa hali ya juu, huku ikiwa ni nishati ya gharama nafuu ili watu wengi waweze kuimudu.

Total ipo katika nchi zaidi ya 130, na inafanya kila linalowezekana kuboresha maisha watu wa nchi hizo kiuchumi na kijamii kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira husika.

Total imeanzisha kampeni kabambe utafutaji na uzalishaji wa mafuta kwa kuongeza idadi ya visima vya mafuta huku ikijitahidi kupata nishati endelevu kwa ajili ya Bara la Afrika kwa sasa na baadae. Total imejikita katika uhamasishaji wa utafutaji vya vyanzo vipya vya nishati kutoa kipaumbele cha elimu ya nishati kwa vijana ili kuendeleza uwezo wa kipekee wa bara hili la Afika kujiletea maendeleo. Mbali na hilo,Kampuni ya Total ndio sambazaji wa kwanza wa bidhaa za mafuta (mafuta ya petroli, dizeli, mafuta ya taa , lami, na GPL, nk) katika bara la Afrika. Shukrani kwa mizizi yake ya kihistoria, ubora wa bidhaa na huduma zake, kutoka jumla ya vituo 4200 vya mafuta katika nchi arobaini barani Afrika. Vituo vya mafuta vya Total ni vituo tegemeo kwa wafanya biashara binafsi na wateja wake. Lengo letu ni kuwezesha upatikanaji mkubwa zaidi wa nishati, ambayo pia inahusisha kuendeleza upatikana wa vyanzo vingi na mbadala vya nishati na kwa gharama nafuu - kama vile nishati ya jua, kwa kuuza vifaa vya nishati ya jua

Total tunasikiliza mahitaji ya wadau wetu, na sisi kwenda nao pamoja nao katika kuendeleza maendeleo ya kiuchumi, ajira, elimu na afya.

**www.total.com**

# Wasabato waombea uchaguzi wa Oktoba

**NA Frank Kaundula, MOROGORO**

KANISA la Waadventista Wasabato (SDA) la Kichangani la Mtaa wa Nanenane, Manispaa ya Morogoro limefanya ibada ya kuombea uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba 28, mwaka huu ili taifa lipate viongozi bora na watakaoleta maendeleo.

Ibada hiyo ilifanyika juzi na kuongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Huduma ya Familia Jimbo la Mashariki Kati, Mchungaji James Machage, ambapo alisema lengo la maombi ni Mungu asaidie taifa hili lipate viongozi wazuri.

"Tumeamua kufanya maombi maalumu ya kuombea uchaguzi mkuu wa mwaka huu, ili Mungu asaide taifa hili lipate viongozi bora watakaoendelea kutupa uhuru wa kuabudu kulingana na imani ya kanisa letu la Kisabato nchini," alisema Machage.

Mchungaji Machage alisema mbali na kupata viongozi bora na watakaoendelea kutoa uhuru wa kuabudu, pia maombi hayo yataendana na Mungu kuwasaidia wagombea kuwapa ulinzi katika harakati na safari zao za wakati wa kampeni.

"Wagombea wamekuwa wakisafiri sana kwa lengo la kufanya kampeni, hivyo pia tunamwomba Mungu wetu wa mbinguni awatangulie wagombea hao, ili awaepushe na vizuizi vya aina yoyote ile ikiwamo ajali kwa kuwapa ulinzi," alisema Machage.

Mchangaji Machage alimwomba Mungu awape maneo yenye busara wagombea wote watakapokuwa wakinadi sera zao kwenye kampeni kuepuka chuki ambazo zinaweza kuhatarisha amani iliyopo nchini.

Alisema taifa hili ni nzuri na ni tajiri sana, na limejaliwa kuwa na amani, hivyo wagombea wanatakiwa kulielewa hili kwa mapana zaidi kwa kuepuka lugha mbaya ikayoleta chuki na kusababisha uvunjifu wa amani katika jamii.

Katika hatua nyingine mchungaji huyo aliwataka vijana wa kanisa hilo kuwa wajasiriamali wa aina mbalimbali, ili wajipatie kipato cha kuwawezesha kijikimu kimaisha ambapo pia aliwaonya vijana hao kuishi kwa kutegemea misaada.

Alisema vijana wanatakiwa mfano mzuri katika jamii inayowazunguka kwa kufanya kazi za kijipatia kipato, ili Mungu abariki kazi za mikono yao. Mzee wa Kanisa, Nehemiah Kachemu, alisema kutokana na maombi yaliyofanywa na waumini wenzake SDA, Mungu amesikia hivyo taifa litapata viongozi watakaoongoza nchi kwa hofu ya Mungu.



Kaimu Meneja wa Ukaguzi wa Wakala wa Vipimo (WMA), Almachius Pastory akitoa elimu kwa madereva wa bodaboda, kuhusu jinsi ya kubaini mizani ambayo haijahakikiwa na wakala kwenye mafunzo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wajasiriamali 167 wapewa vyeti vya ubora

**Na Joseph Mwendapole**

WAZALISHAJI wakubwa, wa kati na wajasiriamali 167 wamepatiwa vyeti na leseni vya ubora na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), baada ya bidhaa wanazozalisha kuthibitishwa ubora na kukidhi matakwa ya viwango.

Wazalishaji hao walikabidhiwa vyeti na leseni hizo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBS, David Ndibalema, alisema vyeti na leseni hizo zitawasaidia wazalishaji hao kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kushindana sokoni, kuwaondolea usumbufu wa kupima bidhaa kwa kuzingatia matakwa ya wanunuzi.

"Leseni na vyeti hivyo vitawakinga wazalishaji dhidi ya ushindani na bidhaa duni, hafifu zisizo na ubora, kuongeza imani kwa umma juu ya ubora wa bidhaa iliyothibitishwa, hivyo kumpatia wateja wengi zaidi na kuingia na kuuzwa katika soko la Afrika Mashariki pasipo kufanyiwa vipimo zaidi," alisema Ndibalema.

Ndibalema alisema leseni na vyeti hivyo vinathibitisha kuwa bidhaa husika inafaa kwa matumizi husika na kumhakikishia mtumiaji usalama wake kiafya na kulinda mazingira.

Mkurugenzi huyo aliwapongeza wazalishaji wakubwa, wakati pamoja na wajasiriamali waliofanikiwa kupata vyeti na leseni za kutumia alama ya ubora.

Aliishukuru serikali kwa kuwahudumia wajasiriamali wadogo kupitia huduma za shirika hilo juu ya udhibiti ubora bila malipo ya gharama za ukaguzi na upimaji.

Ndibalema aliwataka wajasiriamali hao kuhifadhi vizuri kumbukumbu zao za uzalishaji na mauzo ili ziwasaidie wakati wa tathmini.

Katika hatua nyingine, Ndibalema alisema katika kipindi cha kuanzia Aprili hadi Juni mwaka huu wamesajili majengo 1,812 ya biashara na ya kuhifadhi bidhaa za vyakula na vipodozi na bidhaa 445 za vyakula na vipodozi.

Kwa mujibu wa Ndibalema, jukumu la usajili wa vyakula, vipodozi na majengo limetokana na marekebisho ya sheria ya viwango yaliyofanywa na Sheria ya Fedha ya mwaka 2019.

# Sababu mfumuko wa bei kubaki 3.3%

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MFUMUKO wa bei wa Taifa, kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti 2020, umebaki kuwa asilimia 3.3 kama ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Julai, 2020.

Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ruth Minja, alibainisha hayo jana jijini Dodoma, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Minja alisema kuwa hali hiyo inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti 2020, imebaki kuwa sawa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia mwezi Julai, 2020.

"Mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti 2020, kuwa sawa na mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Julai 2020, kumechangiwa na kupungua na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula kwa kipindi kilichoishia mwezi Agosti 2020, zikilinganishwa na bei za mwezi Agosti 2019," alisema Minja.

Vile vile, alisema baadhi ya bidhaa za vyakula zilizopungua bei kwa mwezi Agosti 2020, zikilinganishwa na bei za mwezi Agosti 2019 ni mahindi kwa asilimia 5.8, unga wa ngano kwa asilimia 1.1, mihogo kwa asilimia 16.3 na viazi vitamu kwa asilimia 11.9.

"Kwa upande mwingine baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizoongezeka bei kwa mwezi Agosti 2020, zikilinganishwa na bei za mwezi Agosti 2019, ni na mavazi kwa asilimia 2.2, ada za shule za msingi na sekondari za binafsi kwa asilimia 2.4 na huduma za malazi kwenye nyumba za wageni kwa asilimia 2.8," alieleza Minja.

Pia alisema mfumuko wa bei za bidhaa za vyakula na vinywaji baridi, kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti 2020, umepungua hadi asilimia 3.7 kutoka asilimia 3.8 kwa mwaka ulioishia mwezi Julai, 2020.

Aidha, alisema hali ya mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki, unaonyesha Kenya mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti 2020, umebaki kuwa asilimia 4.36 kama ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Julai 2020.

Nchini Uganda, mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishi Agosti 2020, umepungua kidogo hadi asilimia 4.6 kutoa asilimia 4.7 kwa mwaka ulioishia Julai, 2020.

# Shirika lawapa wazee matibabu ya bila malipo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SHIRIKA la Tunajali, linalomiliki zahanati iliyopo Kwamatiasi Kata ya Mkuza Halmashauri ya Mji wa Kibaha, linatarajia kutumia zaidi ya Sh. milioni 2 kwa ajili ya matibabu ya wazee waliogundulika kuwa na ugonjwa wa kisukari.

Wazee hao 17 ni kati ya 417 waliofika katika Zahanati ya Tunajali kwa ajili ya upimaji wa afya na kupatiwa matibabu bure ulioendeshwa na shirika hilo.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Tunajali, Nicas Mawazo, alisema, wamekuwa na utaratibu wa kupima afya wazee, wanawake na watoto lengo likiwa kusogeza huduma karibu na wananchi na kuondoa adha ya kupata huduma hizo.

Nicas alisema katika zoezi lililofanyika mwishoni mwa wiki, wazee 417 walijitokeza kupima afya zao, ambapo 273 waliogundulika kuwa na magonjwa ya macho na 40 kati yao wanahitaji upasuaji mdogo, 17 walikuwa na kisukari na 70 wanahitaji upasuaji wa tezi dume.

Alisema wanaendelea kutoa huduma bure ya matibabu kwa wazee waliogundulika kuwa na kisukari, ambapo gharama yake ni zaidi ya shilingi milionimbili katika hatua ya awali.

Mkurugenzi huyo aliomba wadau kutoka ndani na nje ya mji wa Kibaha kujitokeza kusaidia matibabu ya upasuaji mdogo wa macho kwa wazee pamoja na wazee waliogundulika kuwa na tezidume.

"Nimeandaa utaratibu katika zahanati hii, tuwe tunasaidia makundi maalumu kupata huduma bure za afya, nimewafikia, lakini changamoto niliyonayo ni katika matibabu kwa baadhi ya magonjwa hususani ya upasuaji, ninaomba atakayeguswa atuunge mkono tuwasaidie wagonjwa," alisema Nicas.

Jumanne Ramadhani, mmoja wa wazee waliofika kupata huduma katika zahanati hiyo, aliiomba serikali kuboresha huduma kwa wazee.

Alisema serikali pia inatakiwa kuwaangalia wananchi ambao kipato chao ni cha chini ambao wanashindwa kumudu gharama za matibabu.

Naye Abdul Solomba, alisema inatakiwa kuwafanyia wazee huduma ya kuwapima afya bure kama shirika hilo linavyofanya.

**Serikali pia inatakiwa kuwaangalia wananchi ambao kipato chao ni cha chini ambao wanashindwa kumudu gharama za matibabu.**

# Askofu: Waumini hudhurieni mikutano yote ya kampeni

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

KANISA la Anglikana Dayosisi ya Mara, limewataka waumini wake na wananchi wote kujitokeza kwa wingi katika mikutano ya kampeni ya wagombea wa vyama vya siasa ili waweze kusikiliza sera zao, na siku ya uchaguzi wawachague viongozi watakaowaletea maendeleo.

Kanisa hilo limewataka wananchi wote ambao wamejiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura siku ya Oktoba 28, mwaka huu, wajitokeze kwa wingi kwa ajili ya kuwachagua viongozi wanaowapenda wawe wawakilishi wao.

Aidha, hilo limewataka wagombea wote wa udiwani, ubunge na urais kufanya kampeni za kiungwana na kistarabu na bila kutumia lugha za matusi, uchochezi na mambo mingine ambayo yanaweza kusababisha uvunjifu wa amani.

**Sasa wagombea wengine tunawaona kwenye majukwaa na kwenye mitandao ya kijamii, wanatoa lugha za matusi bila sababu zozote za msingi.**

Hayo yalisemwa jana na Askofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Mara, George Okoth, kwenye Ibada ya Kipaimara, iliyofanyika katika kanisa la Anglikana Parish ya Kabainja Wilaya ya Bunda mkoani Mara.

"Tunawataka wagombea wa vyama vyote wakati huu wa kampeni wafanye kampeni zao kistarabu, kiungwana na bila kukejeli au kutoa lugha za matusi kwa wagombea wengine, bali waseme sera zao kwamba wakichaguliwa watawafanyia nini wananchi," alisema.

"Sasa wagombea wengine tunawaona kwenye majukwaa na kwenye mitandao ya kijamii, wanatoa lugha za matusi bila sababu zozote za msingi."

Katika ibada hiyo baba Askofu Okoth aliwataka watu kukua kiroho kwa kuacha matendo mabaya, yakiwamo ya uzinzi, kutumia dawa za kulevya na pombe, pamoja na mila potofu zikiwamo za ukeketaji watoto wa kike.

Askofu Okoth aliwaasa wanafunzi kuzingatia elimu na kuacha kujiingiza katika vitendo ambavyo vinaweza kusababisha kukatisha masomo yao na kwamba wanaume wakiwatongoza wachukue hatua ya kuwashtaki kwa wazazi wao na kwenye vyombo husika, ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao.



Mgombea ubunge Jimbo la Shinyanga Mjini kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Godwin Makomba, akiomba kura kwa wakazi wa Shinyanga Mjini juzi, katika kampeni za uchaguzi mkuu. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Makato ruzuku TASAF yachochea kasi wasichana kuhudhuria shule

**Na Shaban Njia,** DODOMA

UKATWAJI wa ruzuku kwa wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF) kwa kushindwa kuwahimiza watoto wao kwenda shuleni, kumesababisha ongezeko la wanafunzi hasa wa kike kuhudhuria masomo ukilinganisha na kipindi cha nyuma.

Utaratibu huo umewafanya wazazi na walezi kuhamasika na kuwahimiza watoto wao hasa wa kike kwenda shuleni, ili wasiendelee kukatwa fedha zinazotolewa na mpango wa kunusuru kaya maskini na mpango huo ulianza mwaka 2016 hadi 2017.

Hayo yalibainishwa jana na mtaalamu wa ufuatiliaji na tathmini kutoka TASAF, Fariji Mishael, wakati wa kikao kazi cha kujenga uelewa kwa waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa kipindi cha pili cha awamu ya Tatu ya Tasafu (PSSN II) kutoka mikoa ya Dodoma, Iringa, Singida na Shinyanga kilichofanyika jijini Dodoma.

Alisema tangu kuanzishwa kwa utaratibu huo wamekwisha wakata zaidi ya asilimia 80 kaya maskini, na kuwa na ongezeko la asilimia nne ya wanafunzi kuhudhuria masomo vipindi vyote na kupunguza wimbi la wanafunzi wanaoishia njiani wakielekea shuleni na kurudia rudia masomo kila mwaka.

"Ndungu zangu, bila TASAF umaskini ungeongezeka kwa asilimia mbili sawa na watu milioni 1 zaidi, na umaskini uliokithiri ungeongezeka pia kutoka asilimia nane hadi 9.2 na tungekuwa na wimbi kubwa la vijana wa mitaani wasiokuwa na elimu hasa watoto wa kike," alisema Mishael.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, alisema mwaka jana zaidi ya wanafunzi 377 kutoka kaya maskini maeneo mbalimbali nchini, wamehitimu kidato cha sita na kujiunga na vyuo vikuu na kupata mikopo ya elimu kwa asilimia 100.

Katibu Tawala wa Jiji la Dodoma, Kessy Maduka, alizipongeza kaya maskini zilizoshiriki kikamilifu kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuchangia kodi serikalini na kusababisha nchi kuingia kwenye uchumi wa kati.

Maduka alivitaka vyombo vya habari kuendelea kutoa elimu ya umuhimu wa kodi na tafsiri sahihi ya uchumi wa kati, ili kila mwananchi hasa wanaoishi pembezoni mwa miji watambue maana sahihi ya uchumi wa kati.

# Mawakala CRDB wapewa angalizo utakatishaji fedha

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI mkoani Shinyanga imewaonya mawakala wa Benki ya CRDB kuacha kujiingiza kwenye masuala ya utakatishaji fedha.

Imesema vitendo hivyo vinaweza kuharibu sifa ya benki hiyo pamoja na taifa kwa ujumla ambalo kwa sasa lipo kwenye uchumi wa kati.

Imeelezwa nchi inapoingia kwenye uchumi wa kati, huwa kuna mzunguko mkubwa kibiashara pamoja na wananchi kutumia huduma mara kwa mara za kifedha, ambapo pia matapeli huwa ni wengi, na kuwataka mawakala wa benki ya CRDB kuwa makini wakati wa utoaji huduma kwa wateja wao.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, alibainisha hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa mawakala wa benki ya CRDB ya utoaji huduma bora kwa wateja, kutoka wilaya za Nzega, Kishapu, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, na Manispaa ya Shinyanga, yaliyofanyika Mjini Shinyanga na kukutanisha mawakala 300.

**Mafunzo hayo yatawasaidia kuwa makini wakati wa utoaji huduma kwa wateja wao na kuepuka matapeli na kutojiingiza kwenye masuala ya utakatishaji fedha.**

Alisema serikali inatambua mchango wa taasisi za kifedha katika kukuza uchumi wa taifa na wananchi, pamoja na kupanua wigo wa ajira wakiwamo mawakala ambao hutoa huduma za kifedha kwenye maeneo mbalimbali.

Aliwataka wawe makini wakati wa utoaji wa huduma zao na kujiepusha kujiingiza kwenye masuala ya utakatishaji fedha.

"Nawaasa mawakala kufanya biashara yenu ya uwakala kwa umakini mkubwa, kwani mnapohudumia mteja mnaiwakilisha Benki ya CRDB ambayo inaendesha shughuli zake kwa mujibu wa matakwa ya Benki Kuu, hivyo mkiharibu mnaichafua Benki ya CRDB na taifa kwa ujumla," alisema Telack.

"Hivyo nawaomba muwe makini sana hasa katika kipindi hiki ambapo nchi ipo kwenye uchumi wa kati, na kutojiingiza kwenye masuala ya utakatishaji fedha... mtu akileta mamilioni ya fedha mhoji kwanza amezitoa wapi, akileta ubabaishaji toa taarifa na usiwe sehemu ya kushiriki uhujumu uchumi," aliongeza.

Pia aliwaonya mawakala hao wasijiingize kwenye biashara za ukopeshaji kwa kutoza riba kubwa, ambazo ni kandamizi kwa wananchi wakiwamo na wafanyakazi, na kukamata kadi zao za ATM kutokana na kushindwa kurejesha marejesho.

Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Magharibi inayounda mikoa ya Shinyanga, Tabora, Kigoma, Geita na Wilaya ya Sengerema, Saidi Pamui, alisema wameendesha mafunzo hayo ya utoaji huduma bora kwa mawakala wa benki hiyo, pamoja na kuwa makini hasa katika kipindi hiki, ambapo Tanzania imeingia kwenye uchumi wa kati, ili wasijiingize kwenye masuala ya utakatishaji fedha.

Mmoja wa mawakala hao, Jamila Kilangi, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kuwa makini wakati wa utoaji huduma kwa wateja wao na kuepuka matapeli na kutojiingiza kwenye masuala ya utakatishaji fedha.




Meneja Mawasiliano wa Tigo Tanzania, Woinde Shisael, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa huduma mpya ya "Chukua Kilicho Chako", itakayompa mteja wa kampuni hiyo uwezo wa kurefusha muda wa matumizi ya kifurushi ambacho kinakaribia kufikia ukomo wa muda wake wa matumizi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC aonya uchomaji moto miundombinu ya umeme

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

SERIKALI ya Wilaya ya Morogoro imeeleza kusikitishwa na kitendo cha baadhi ya wananchi kuchoma moto katika maeneo ya hifadhi za miundombinu ya umeme, jambo linalohatarisha usalama wa miundombinu hiyo na watumiaji nishati ya umeme.

Mkuu wa wilaya hiyo, Bakari Msulwa, alisema uharibifu huo unafanywa na baadhi ya wananchi wanaojihusisha na shughuli za kilimo maeneo ya hifadhi za njia ya umeme.

Alisema moto huo uliwashwa katika maeneo ya Kingolwira na Msamvu jirani na kituo cha kupozea umeme ambapo alilazimika kutoa melekezo ya serikali ya kutaka wahusika wote kutafutwa na kuchukuliwa hatua.

"Kitendo hiki cha kuwasha moto katika maeneo ya hifadhi ya miundombinu ya umeme ni hatari sana hasa katika eneo hili la Msamvu jirani kabisa na kituo cha kupozea umeme, lakini nguzo zikiwaka moto na kuanguka zitafanya maeneo mengi kukosa umeme," alisema Msulwa.

Msulwa aliwataka wananchi kwa kushirikiana na watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoa wa Morogoro katika kuwatambua waliofanya kitendo hicho ili kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Kelvin Kapinga, Ofisa Usalama wa TANESCO Mkoa wa Morogoro, aliwashukuru wasamaria wema waliotoa taarifa mapema juu ya moto uliowashwa katika maeneo hayo na kuchukua hatua za haraka kuuzima ili usilete madhara makubwa.

"Nawashukuru baadhi ya watu walitoa taarifa mapema kabla madhara makubwa hayajatokea pamoja na kusaidia kuzima kama wasingefanya hivyo serikali yetu ingepata hasara kwa miundombinu hii kuharibika," alisema Kapinga.

# TADB kuleta fursa pamba Kanda Ziwa

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

MKOPO wa zaidi ya Sh. bilioni 11 wa masharti nafuu ambao umetolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB) unawanufaisha wakulima wa pamba katika maeneo ya Kanda ya Ziwa.

Maeneo hayo ni Chato, Biharamulo, Kahama, Msalala, Ushetu na Muleba.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS- Chato), Elias Kaswahili, alibainisha hayo jana na kueleza kuwa:

"Mkopo wa TADB umetuinua kimaisha pamoja na kuongeza ufanisi katika utendaji kwa kuwa tumefanikiwa kupata ofisi na vitendea kazi vingine ikiwamo trekta. Fedha hii pia imekuwa ikirahisisha ukusanyaji wa zao hilo katika maeneo mbalimbali."

Alisema pia TADB imewapa mashine ndogo ndogo za kusindika mazao ya pamba na alizeti.

Wakulima wananufaika kutokana na uzoefu ambao umejengwa na vyama vyao vya ushirika katika kusimamia fedha inayotolewa na TADB toka msimu wa kilimo wa 2012/2013.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema benki hiyo imedhamiria kurudisha thamani ya zao la pamba, ili kuendelea kuwanufaisha wakulima wa Kanda ya Ziwa ambao wamekuwa wakilitegemea zao hilo kujipatia mapato kwa kipindi kirefu cha nyuma.

"TADB tumekuwa na malengo ya kuhakikisha wakulima, wavuvi na wafugaji kote nchini wananufaika na mikopo yenye masharti nafuu, ili kuongeza thamani kwa mazao yanayotokana na mifugo, uvuvi na kilimo," alisema na kuongeza:

"Tumetoa zaidi ya Sh. bilioni 11 ili kurejesha thamani ya zao la pamba kwa wakulima wa Kanda ya Ziwa na kuwahakikishia upatikanaji wa soko."

Ameeleza kuwa mkopo huu utasaidia wakulima kupata malipo ya mazao yao kwa wakati, kuhuisha utendaji wa vyama vya ushirika pamoja na upatikanaji wa ajira za muda mfupi na mrefu jambo ambalo litasaidia kuinua mapato ya mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.


"Mpango wetu ni kuwafikia wakulima wengi zaidi, dhamira ambayo tutaikamilisha kupitia ushirikiano tulionao na benki washirika.

Mpaka sasa zaidi ya wakulima 15,000 wamenufaika moja kwa moja na mkopo huu na tumekuwa na malengo ya kuwaunganisha wakulima wengi zaidi katika mnyororo huo wa thamani," alifafanua.

## Wafanyabiashara EAC sasa waitaka Congo A/Mashariki

Ukurasa 12





siasa
JUMATANO SEPTEMBA 9, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

Ukurasa 14

## P W BOTHA

# Kwa sheria hizi rushwa uchaguzi inatoka wapi?

Na Gaudensia Mngumi

KARIBUNI imeonekana video kwenye mitandao ikionyesha wanawake wanaolalamikia uchaguzi wa diwani wakiuhusisha na vitendo vya ukosefu wa maadili kwenye uchaguzi.

Wanamtuhumu mgombea mwanamama kuwa anadai ametumia mwili wake kupata udiwani na wanahisi kuwapo kwa vitendo vya rushwa ya ngono katika uteuzi wake.

Wananchi wanalalama na wanaeleza jinsi mgombea udiwani huyo alivyotukana wenzake kuwa hawajaweza kufanikiwa kwa sababu hawajaitoa miili yao kupata uongozi bwerere.

Wakati huu wa uchaguzi ni muhimu wapigakura na raia kuelewa kuwa ajenda muhimu ya uchaguzi ni maendeleo, hivyo vikwazo vinavyokwamisha uchaguzi ni adui wa maendeleo na rushwa ni miongoni mwa mambo yanayochangia.

Rushwa inatajwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwa ni adui wa uchaguzi ulio huru na haki.

Hayo yanajiri kwenye mkutano wa wanahabari na wadau wa asasi za kirai wa kufanya tafakuri ya uchaguzi wa Oktoba 2020, walipokutana Dar es Salaam.

Ofisa wa taasisi hiyo, Matai Kirumbi, anasema rushwa ni tatizo linalozikabili nchi nyingi duniani ikiwamo Tanzania na inatumiwa kwenye maeneo mengi wakati wa uchaguzi.

Anasema kwa mfano wapo wanaoitoa ili kushawishi kuteuliwa na vyama kugombea nafasi fulani. Lakini pia, inatolewa kwa baadhi ya wapigakura ili kupiga au kutopiga kura na huko ndiko kuua ajenda ya maendeleo.



Ajenda ya uchaguzi na kupiga kura ni kupata maendeleo. **PICHA: MTANDAO.**

Aidha, anasema inatumika kushawishi wagombea wengine kujitoa au kujiingiza katika mchakato wa uchaguzi ili kupunguza au kuongeza ushindani.

Kadhalika, Kirumbi anawaeleza washiriki kuwa inatumika katika hatua ya kuhesabu kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi. Yote hayo yana athari mbalimbali kwenye mchakato ulio huru na haki na azma ya kufikia maendeleo.

### ATHARI ZA UCHAGUZI

Mfano, Kirumbi anasema rushwa katika, uchaguzi inaondoa uhuru wa wapiga kura, baadhi huchagua viongozi kwa kigezo cha hongo waliyopokea.

Nyingine kwa mujibu wa maelezo yake ni kupoteza dhana nzima ya uchaguzi ulio huru na haki.

Ndiyo inayosababisha, wagombea wenye uwezo wa kuwakilisha na kuongoza jamii na taifa hushindwa kushiriki kugombea katika uchaguzi kwa kukosa fedha kutokana na imani kwamba bila ya kuwa na fedha hawataweza kuhonga wananchi ili wamchague au kuwachagua.

### KUPOTEZA HAKI

Ofisa huyu wa TAKUKURU anasema rushwa katika uchaguzi inasababisha viongozi wala rushwa kuingia madarakani. Aidha, watu hao waliochaguliwa kwa njia ya mlungula hawawezi kusimamia na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa.

### VIPI KUHUSU SHERIA?

Uchaguzi ni mchakato ambao unasimamiwa kikatiba na kisheria. Zipo sheria nyingi zinazousimamia ili uwe huru na haki lakini mbona kelele za mlungula zipo? Inakuwaje Watanzania waendelee 'kuona mchakato huo kuwa ni kipindi cha kuvuna'?

Sheria zinazokataza rushwa ni nyingi hivyo ni wakati wa kuzijua na kuzifuatilia ili kuhamasishana kupinga vitendo vya ukosefu wa maadili kwenye uchaguzi.

Sheria hizo ni pamoja na ile ya Uchaguzi Namba 1 ya mwaka 1985 sura 343, inayoweka taratibu za uchaguzi na vitendo vinavyokatazwa.

Ipo Sheria ya Vyama vya Siasa Namba 5 ya mwaka 1992, sura 258 inasimamia na kudhibiti mienendo ya vyama

Aidha sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007 inayodhibiti vitendo vya rushwa hata kwenye mchakato wa uchaguzi. .

Kadhalika kuna Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 ambayo imeweka mipaka katika matumizi ya fedha kwenye mchakato wa uchaguzi na kuainisha mambo yote yanayokatazwa.

Hizi ndizo ambazo wananchi na wapigakura wanatakiwa kuzifahamu na kuzitumia wakati wa uchaguzi kwa sababu ajenda ya mchakato huo ni rushwa ni adui wa maendeleo yao na taifa.

Tanzania kwa mujibu wa katiba ina uchaguzi wa aina mbili, uchaguzi mkuu na wa serikali za mitaa. Wa serikali za mitaa unaohusisha kuchaguliwa kwa viongozi wa mitaa, vijiji na vitongoji. Unafanyika chini ya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Namba 4 ya mwaka 1979 (Sura 292).

Kwa sasa kitakachofanyika ni uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani unaofanyika kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi namba 5 ya mwaka 1985 na pia unatajwa kwenye katiba..

Kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika mwishoni mwa mwaka jana, licha ya kusimamiwa na sheria pia kuna kanuni za kuusimamia zinazokataza mambo yasiyoruhusiwa kufanyika na chama au mgombea kwenye mchakato wa uchaguzi ambayo ni pamoja na kutoa rushwa ili kumshawishi yeyote kupiga kura, kugombea au kujitoa katika kugombea nafasi ya uongozi. Aidha, kanuni zinakataza kukodi au kutumia usafiri wa aina yoyote kubeba na kusafirisha wapiga kura kwa madhumuni ya kushawishi kupigiwa kura.

Halikadhalika, kanuni zinakataza kununua kura au kutoa rushwa ya aina yoyote ya fedha au vifaa kwa mpiga kura au Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Pamoja na hayo Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya 2007 nayo inakataza mambo yote yanayohusisha kutoa kitu kidogo kwenye uchaguzi.

Kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya 2007 kinazungumzia kuhusu hongo kikitamka kuwa mtu yeyote atakuwa ametenda kosa la rushwa iwapo, atashawishi, atapokea au atajaribu kupokea kutoka kwa mtu yeyote kwa ajili yake mwenyewe au mtu mingine manufaa, zawadi au vinginevyo ....

Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, pamoja na kusimamia mchakato wa uchaguzi mkuu, inaharamisha rushwa, ikisema ni kosa: kutoa rushwa kwa mgombea ili kumshawishi ajitoe kwenye kugombea.

Aidha kutoa rushwa kwa wapiga kura ili kuwashawishi wampigie kura mgombea fulani au waache kupiga kura.Pia, inakataza kutoa takrima.

Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 katika kifungu cha 21 (I) 'a hadi g' inaainisha makatazo ya mgombea au wakala wake, vyama vya siasa au mwananchi wakati wa mchakato wa uteuzi, kampeni au uchaguzi:

Anakataza kutoa fedha au kukopesha au kuahidi kitu chochote chenye thamani ili kupigiwa kura.

Wakati huo huo, Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 inakataza kutoa au kusaidia kutoa ajira au wadhifa sehemu za kazi ili kupigiwa kura.

***ITAENDELEA***

# Wafanyabiashara EAC sasa waitaka Congo A/Mashariki

**Na Nimi Mweta**

JUHUDI zimeanza miongoni mwa wadau wa biashara wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kutaka kikao cha wakuu wa nchi kiruhusu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) iweze kujiunga na EAC.

Rai hiyo inatolewa kwa nguvu hivi karibuni na uongozi wa Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC), ikisema kuwa uanachama wa DRC utasaidia kuongeza tija kwa nchi wanachama. Ni suala ambalo inaelekea halitakuwa rahisi kwa wakuu wa nchi kulitatua, ila huenda lina mashiko.

Akiwasilisha ombi hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa EABC Dk.Peter Mathuki, hakueleza kwa undani kama DRC inafikia kikamilifu vigezo vya kupata uanachama wa EAC, ila alitaja kuwa nchi hiyo inapakana na nchi zote wanachama.

Anaweka mkazo zaidi katika wingi wa fursa ambazo Congo ingezingiza endapo biashara na wanachama itarahisishwa kwa kuingia rasmi katika Jumuia.

Hapakuwa na ubishi kuhusu hoja hizo ila bado ina vizingiti vya sifa za uanachama na kimkakati, uwiano au mizania kati ya fursa na vihatarishi.

Kwa mujibu wa Dk. Muthuki kampuni ndogo na za kati zinazofuatilia biashara DRC zitaongeza wigo wa shughuli hizo kwani taratibu nyingi za kuingiza na kutoa bidhaa zitakuwa zinaendeshwa kwa msingi wa kanuni za Jumuia ya Afrika Mashariki.

Ni nyenzo ya kuondoa urasimu na hasa rushwa, kwani taratibu za biashara za ndani ya nchi moja inabidi zitafsiriwe na wasimamizi wa sekta husika zinalenga kufanya nini? Zinahusisha nini au zinazuia kitu gani? Wakati zile za nchi kadhaa zinaeleweka kwa urahisi zaidi.

Mifumo ya soko la pamoja ni urasimishaji wa kanuni za kimataifa za biashara, kuondoa urasimu ambao unazuia ushindani; rushwa izuiwe kirahisi zaidi.

Tayari DRC ilishafikisha maombi ya uanachama wa EAC Juni mwaka jana, ambayo ina maana kuwa suala hilo lilishaanza kujadiliwa lakini kuna vizuizi, ndiyo maana baraza hilo linataka viondolewe. Watalaamu katika sekretariati ya EAC, Baraza la Mawaziri na hata wakuu wa jumuia tayari watakuwa wamelijadili suala hilo, bila kufikia muafaka kuikubalia DRC uanachama.

Mojawapo ni hali tete ya amani nchini humo, kuwa urahisi wa wananchi wake kuingia na kutoka nchi nyingine za Afrika Mashariki kunaweza kurahisisha kujenga maskani mapya na kuzidisha uwezo wao wa kuharibu amani.

Ina maana kuwa nchi wanachama zenye mpaka na DRC nazo zingekuwa hatarini kuathirika na hali hiyo, endapo wataalamu wanasema ni wazi itakuwa hivyo. Siyo rahisi kuthibitisha na mara nyingine tahadhari hiyo inaweza kuwa ni hofu.

Baraza hilo linaelewa fika kuwa ziko changamoto za kisiasa kuhusu uanachama wa DRC, lakini kama ilivyo kwingine inaaminika kuwa uboreshaji wa shughuli za kibiashara na kupanua wigo wa matazamio kiuchumi ndani ya Congo unaweza pia kuleta athari chanya kwa mustakabali wa kisiasa nchini humo.



Uvuvi wa samaki katika Ziwa Tanganyika ni moja ya biashara inayoendelea baina ya wafanyabiashara wa Tanzania na Congo. **PICHA: MTANDAO**

Taifa hilo ni kubwa kwa eneo na hata idadi ya watu, kwa wakazi wake wanafikia milioni 80 na ina vianzio vingi vya utajiri hasa madini na mahitaji mengi ya bidhaa zinazopatikana miongoni mwa wanachama wa EAC.

Isitoshe Jumuiya ya Afrika Mashariki ndiyo eneo kubwa zaidi linalopakana na DRC kibiashara, ukilinganisha na kwingineko.

Congo Brazaville kwa upande wa magharibi, Jamhuri ya Afrika ya Kati Kaskazini na hata Angola na Zambia kusini magharibi yanaweza kuwa maeneo muhimu kwa baadhi ya majimbo ya DRC lakini EAC ni sehemu muhimu kwa upande wake wa mashariki, kati, kaskazini na kusini mashariki.

Aidha wakazi wa DRC wana mahusiano ya kina na nchi za EAC hasa kwa upande wa lugha ambako wengiCongo wanaongea Kiswahili bila matatizo.

Kitaifa au kwa makabila pia wamechanganyika sana, na kisiasa iko maingiliano mengi zaidi ambayo pia yanaweza kusaidia kutatua shida zilizopo Congo kwa sasa ni biashara na uthubutu.

Mustakabali wa kisiasa wa nchi hiyo kwa sasa unaelekea ndiyo tatizo la msingi la kupata uanachama

> “Mojawapo ni hali tete ya amani nchini humo, kuwa urahisi wa wananchi wake kuingia na kutoka nchi nyingine za Afrika Mashariki kunaweza kurahisisha kujenga maskani mapya na kuzidisha uwezo wao wa kuharibu amani.

EAC,lakini baadhi ya wataalamu wanakumbusha kuwa taifa hilo lilifanya uchaguzi mkuu mwisho wa 2017 ambao licha yakuwa na upungufu kadhaa, umeweka misingi thabiti ya kuendeleza demokrasia. Wataalamu wa siasa ‘geopolitik’wa Afrika Mashariki wanaona kuna uwezekano msingi huo kuboreshwa zaidi endapo njia za uchumi zinafunguka kwa upana zaidi nchini humo kupitia mahusiano ya karibu zaidi na nchi za EAC.

Maeneo yenye watu wengi na vianzio bora zaidi vya uwekezaji, urahisi wa usafirishaji nje, bado ni upande wa mashariki, yaani EAC.

Kushirikiana na Afrika Mashariki kunaweza pia kutoa msukumo kwa DRC kuweka miundombinu bora zaidi ya kitaasisi kwa mfano katika biashara ya madini, kama Rais John Magufuli alivyofanya kwa Tanzania.

Miundombinu hiyo ikiboreshwa inaweza kuwa sehemu ya soko la kimataifa la bidhaa adimu za madini, hata iwe ni kwa kufungua matawi ya soko la madini kama ilivyo Tanzania.

Nchi hizi mbili kwa mfano zikiweza kuunda utaratibu wa uendeshaji soko hilo kwa tarehe zinazowiana kupunguza taabu ya wanunuzi kutoka mbali kusafiri mara kadhaa na kupunguza ulanguzi na utoroshaji wa madini, kuwalipa wachimbaji fedha kiduchu .

> “Congo Brazaville kwa upande wa magharibi, Jamhuri ya Afrika ya Kati Kaskazini na hata Angola na Zambia kusini magharibi yanaweza kuwa maeneo muhimu kwa baadhi ya majimbo ya DRC lakini EAC ni sehemu muhimu kwa upande wake wa mashariki, kati, kaskazini na kusini mashariki.

# NI MAPYA URAIS 2020

## •Mgombea kukampeni na guta, baiskeli
## •Wapuuza 'vikongwe' wataka uhuru, haki




Mgombe urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya Chama Cha Sauti ya Umma (SAU), Muttamwega Mgaywa (kulia) na mgombea mwenza Satia Mussa, baada ya kuchukua fomu za kuwania nafasi hiyo. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

UCHAGUZI mkuu wa Oktoba mwaka huu, unashuhudia sura mpya za wagombea urais wakiwamo kinamama wawili wanaowania safari ya kuingia ikulu.

Wageni hao wameshapitishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), baadhi ya wanasiasa hao ni Naibu Katibu Mkuu wa ADC, Queen Sendga, Cecilia Mwanga kutoka Demokrasia Makini na Philip Fumbo DP, Yeremia Maganja wa NCCR- Mageuzi na Leopold Mahona wa NRA.

Katika kundi hilo, wapo wanasiasa kama; Twalib Ibrahim UPDP, Mazrui Mohamed UMD na Seif Maalim Seif wa AAFP wakati Muttamwega Mgaywa, anakiwakilisha chama cha SAU.

Miongoni mwa sura hizo, mbili siyo mpya sana bali siyo maarufu katika siasa kama walivyo wagombea wa CCM, CUF, CHADEMA na ACT-Wazalendo.

Muttamwega Mugaywa ni miongoni mwao, kwa kuwa amewahi kuwa mbunge kwa kipindi cha miaka 10 na pia amewania urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2010.

Katika uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi mwaka 1995, alichaguliwa kuwa mbunge wa Mwibara, Bunda mkoani Mara.

Wakati huo alikuwa katika Chama cha NCCR-Mageuzi, kisha mwaka 2000, mwanasiasa huyo aliukwaa ubunge wa jimbo hilo kupitia Chama cha TLP, uchaguzi mkuu wa mwaka 2010, aliwania urais.

Baada ya hapo Mugaywa aliyekuwa miongoni mwa wabunge vijana wakati huo, hakusikika tena katika siasa hadi hivi karibuni alipotangazwa kuwa anawania urais kupitia SAU.

Akizungumza na Nipashe anasena kimya chote kilitokana na kujipanga upya kisiasa, kwa vile siasa inataka mikakati, hivyo yupo SAU kuendeleza harakati zake za kisiasa alizozianza miaka ya 90.

Naye mgombea wa NCCR-Mageuzi, Jeremia Maganja, alikuwa Mwenyekiti wa Ngome ya Wazee ya Chama cha ACT- Wazalendo, lakini akahama wakati wa mchakato wa uchaguzi wa viongozi na kujiunga na ngome ya NCCR-Mageuzi.

Mwingine ni Leopold Mahona ambaye ni miongoni mwa wagombea wa nafasi ya urais, kutoka vyama vidogo nchini, aliyewahi kugombea ubunge jimbo la Igunga mkoani Tabora kupitia CUF.

### AHADI ZA WAGOMBEA

Muttamwega anasema, kupitia uzoefu wake katika siasa atasimamia maadili ya vyama vya siasa wakati wote, kwa madai kwamba SAU haipo kwa ajili ya upinzani tu, bali kufika Ikulu na kuleta mabadiliko.

"Kupitia uzoefu wangu katika siasa, nitasimamia maadili ya vyama vya siasa wakati wote ili kufikia malengo ya chama chetu kwani kinalenga kutinga Ikulu na kuleta mabadiliko," anasema Muttamwega.

Maganja anaanisha baadhi ya vipaumbele vya chama hicho ambavyo atavishughulikia iwapo atachaguliwa kuwa ni masuala yote yanayowahusu wakulima, wavuvi na wafugaji.

"Si hao tu, bali hata wafanyabiashara, wafanyakazi ambao wengi wao wanakosa stahiki zao na hata kushindwa kupandishwa madaraja na kuinua uchumi wa kweli wa Mtanzania," anasema Maganja.

### MGOMBEA ADC

Kwa upande wake mgombea wa ADC, Queen Sendiga, kuboresha sekta ya elimu, afya na ya kilimo ndiyo vipaumbele vyake.

"Vipaumbele vyangu endapo Watanzania watanipa ridhaa ya kuongoza nchi, nitaanza na elimu kwa kuboresha maslahi ya walimu, ikiwamo mishahara na makazi. Aidha, nitaongeza vituo vya afya na kusomesha wataalam wengi zaidi ili kulisaidia taifa kwenye kuimarisha maisha na afya bora", anasema Queen.

Anasema, chama chao kinazingatia usawa wa kijinsia na ni moja ya kipengele muhimu kwenye katiba yao, na kwamba mwaka huu pia kuna mwamko mkubwa kwa wanawake kuwania nafasi za uongozi.

### KAMPENI ZA BAISKELI

Wakati Queen akiahidi hayo, mwanamama mwingine Cecilia Mwanga wa Chama cha Demokrasia Makini, anaahidi kufanya kampeni zake kwa kutumia baiskeli au guta.

Analenga kuboresha kilimo ili kiwe na tija.

"Nataka kuudhihirishia umma kwamba watakaponichagua, nitahakikisha nawasimamia watu wa hali chini, wakulima, hatutawabagua tunataka kunyanyuka nao, na tumejipanga na chama chetu," anasema Mwanga.

### KUHIMILI KISHINDO

Mchuano mkali kwenye nafasi hiyo ya urais, unaelezwa kuwa huenda utakuwa kati ya wagombea kutoka katika vyama vya CCM, CHADEMA, ACT-Wazalendo, huku vingine vikisindikiza.

Hata hivyo, baadhi ya wagombea ambao si maarufu kwenye siasa za Tanzania wanatamba kwamba umaarufu wagombea wa vyama hivyo hauwezi kuwababaisha, bali cha muhimu ni uchaguzi kuwa huru na wa haki.

Mgombea urais wa NRA Leopold Mahona, anasema, hatishwi na vyama vikubwa kama CCM, CHADEMA, ACT-Wazalendo wala CUF, kwa maelezo kuwa cha muhimu ni uchaguzi kuwa huru na wa haki.

"Uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, 2020 unatakiwa uwe huru na haki ili Watanzania wachague kiongozi wanayeumtaka, siwezi kuogopa kwamba kuna vyama vikubwa," anasema Mahona.

Philipo Fumbo wa DP, anasema Watanzania wataka sera siyo ukubwa wa vyama, ambapo anaahidi ushindi kwa wanachama wa chama chake, na kutilia mkazo sera zao ambazo zinawabeba watu wenye hali duni.




Mwenyekiti wa NEC, Jaji Mstaafu Semistocles Kaijage, akizungumza hivi karibuni, wakati wa utoaji wa fomu za kuwania urais kwa wagombea kutoka vyama mbalimbali vya siasa, jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

# P W BOTHA

- Kinara ubaguzi, mwasisi mageuzi
- 1986 alitabiri uongozi wa Mwafrika
- Utabiri ukawa Mandela mwaka 1994

**Na Mwandishi Wetu**



Nelson Mandela



Pieter Willem Botha

PIETER Willem Botha, Waziri Mkuu kisha Rais wa Afrika Kusini, historia inamtaja kuwa ni mwanasiasa 'shupavu' akitetea ubaguzi wa rangi na ukandamizaji, lakini wakati ulipofika alibadilisha gia na kuwaambia makaburu mageuzi hayaepukiki. Ukawa mwanzo wa kuwa na Afrika ya Kusini ya Waafrika na Wazungu.

Ni kiongozi aliyetetea hatua zote za kibaguzi za serikali yake kila mahala ingawa alitambua mageuzi yamefika.

Akiwa rais aliishangaza dunia mwaka 1986, aliposema Afrika Kusini siku moja itaongozwa na mtu mweusi.

Kimataifa Botha alikuwa mwakilishi bayana wa mfumo wa ubaguzi wa rangi na mtengano katika wakati ambao utawala huo ulikuwa ukilaumiwa na kulalamikiwa na kuwekewa vikwazo vya kimataifa, yote hayo yalikwisha baada ya Frederck de Klerk, aliyekuwa Rais baada ya Botha kuruhusu uchaguzi huru na Nelson Mandela kuwa rais wa kwanza mweusi wa taifa hilo mwaka 1994.

Alizaliwa Januari 12, 1916 na kufariki dunia Oktoba 31, 2006, akiwa na miaka 90. Ndiye Waziri Mkuu na Rais wa Afrika Kusini, kinara wa ubaguzi wa rangi , tena akijulikana kama "P.W." na "Die Groot Krokodil" kwa lugha ya Kiafrikaana kwa Kiswahili "mamba mkuu".Botha mwenye asili ya makaburu alikuwa Waziri Mkuu kati ya 1978 na 1984.

Botha anatajwa kuwa kinara ya ubaguzi wa rangi, alisimamia kutengeneza bomu la nyuklia nchini Afrika Kusini na upanuzi wa jeshi la taifa.

### MAISHA KISIASA

Alizaliwa katika jimbo la Orange Free State na kusoma sheria katika Chuo Kikuu cha Bloemfontein kuanzia 1932 hadi 1935 lakini aliondoka kable ya kupata shahada na kuanza harakati za kisiasa na kuhamishia makao yake kwenye jimbo la Cape akiwa na miaka 20 akawa mtendaji wa chama tawala cha National Party.

Alichaguliwa kuwa mbunge wa NP kuanzia mwaka 1948, ilipofika 1958 alikuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani , alikuwa Waziri wa Masuala ya Biashara, Ujenzi na Waziri Mkuu B.J. Vorster, alipojiuzulu mwaka 1978 Botha alikuwa Waziri Mkuu wa Afrika Kusini.

Serikali yake ilipata kibano baada ya uhuru wa Angola, Msumbiji na Zimbabwe zote ziliongeza nguvu kwa Waafrika wa Afrika Kusini kudai haki zao na ilikuwa lazima ubaguzi ubadilike.

### ALIJIPAMBANUA TOFAUTI

Katika siasa ya ndani W.P Botha anakuwa na msimamo wa kupunguza kidogo ukali wa ubaguzi wa rangi. Alifuta sheria zilizopiga marufuku ndoa kati ya watu wa rangi mbalimbali (weusi na weupe) lakini akaruhusu vyama vya kisiasa vya watu wa rangi mbalimbali. Alipunguza pia ukali wa "Group Areas Act" sheria iliyokataza watu weusi kuishi katika eneo la wengine rangi nyeupe. Lakini, aliendelea kutazama chama cha wapigania uhuru wa Afrika Kusini cha ANC kama kikundi cha kigaidi akikataa kushauriana na viongozi kama Nelson Mandela. Alikuwa kinara wa kuvuruga amani na kuendesha vita vya kukwamisha uhuru nchini Msumbiji na Angola.

Ilipofika 1989 alilazimishwa kujiuzulu baada ya kuugua na mfuasi wake Frederik W. de Klerk, aliongoza nchi na baadaye kuruhusu uchaguzi huru wa kwanza nchini humu na kutangaza mwisho wa ubaguzi wa rangi

### WOSIA WAKE

Alisema mustakabali wa Afrika Kusini utakuwa mwema iwapo Waafrika na Wazungu wataungana" "Inatunabidi tufanikiwe. Dunia inataka tufanikiwe. Katika enzi za ubaguzi wa rangi na kutengamana zinatoweka.Itakuwa kioja kikubwa na balaa kama wa-Afrika Kusini watashindwa kujiunga pamoja na kukubaliana kusonga mbele. Kuigeuza nchi yao iwe ya kidemokrasi, kama tulivyostahiki kuwa na kupata sifa ambazo nchi yetu inastahiki."

### KUJIUZULU URAIS

Agosti 14, 1989 Pieter Willem Botha, alijiuzulu uraisi baada ya miezi saba ya kutoonekana ikulu kutokana na ugonjwa wa kiharusi. Wakati anaondoka Afrika Kusini iliongozwa na F.W. de Klerk, aliyechukua nchi wakati kukiwa na vuguvugu la mabadiliko na kufunguliwa kutoka gerezani kwa Nelson Mandela.

> "Kaka zangu na dada zangu, Pretoria imetengenezwa na weupe kwa ajili ya watu weupe na hatuna haja ya kuuthibitishia umma au kumthibitishia mtu mweusi kuwa sisi ni bora,tumekuwa tukiwaambia weusi jambo hili mara elfu. Afrika ya Kusini ya leo haikutengenezwa katika mawazo ya kawaida, tumeitengeneza kwa kutumia akili nyingi, jasho na damu. Mnaposema kuwa tunawabagua weusi sielewi. Hivi ni makaburu waliojaribu kusitisha kizazi...

### HOTUBA ZA KIBAGUZI

P.W. Botha anasikika akifagilia ubaguzi ni katika hotuba kwa Baraza la Mawaziri ya Agosti 18, 1985 iliyochapishwa na gazeti la SUNDAY TIMES nchini humo, anasema:

"Kaka zangu na dada zangu, Pretoria imetengenezwa na weupe kwa ajili ya watu weupe na hatuna haja ya kuuthibitishia umma au kumthibitishia mtu mweusi kuwa sisi ni bora,tumekuwa tukiwaambia weusi jambo hili mara elfu. Afrika ya Kusini ya leo haikutengenezwa katika mawazo ya kawaida, tumeitengeneza kwa kutumia akili nyingi, jasho na damu. Mnaposema kuwa tunawabagua weusi sielewi. Hivi ni makaburu waliojaribu kusitisha kizazi cha Waaborijini wa Australia? Je, waliwatenga na kuwanyanyasa watu weusi Marekani kwa kuwaita 'waniga'?

Je, ni makaburu waliowatenga na kuwanyanyasa weusi huku Uingereza kwakuwatungia sheria za kuwakandamiza? Kanada,Ufaransa, Urusi na Japani nao wana njia zao za kibaguzi. Hivi kwa nini kuna kelele nyingi dhidi yetu? Huu ni wenda wazimu! Kwa nini wanatukaba koo kiasi hiki? Hawatutendei haki hata kidogo.Nataka kuwaeleza kuwa hakuna kibaya tunachokitenda hapa ambacho hao wanaojiita wako katika dunia ya ustaarabu wameacha kukifanya. Sisi ni watu wema tusio na hatia na ambao tumeweka wazi mfumo wa maisha tunayotaka tuishi kama watu weupe. Sisi sio wanafiki kama wazungu wenzetu wafanyao kama kwamba wanawapenda watu weusi.Ukweli kuwa watu weusi wanafanana na binadamu na kutenda mambo kama binadamu hauhalalishi wao kuwa wenye akili timamu au binadamu waliotimia.

Karunguyeye si nungunungu na mijusi hawawezi kuwa mamba eti kwa sababu tu wanafanana.

Kama Mungu angelitaka tufanane na watu weusi angetufanya sote tuwe na rangi na fikra sawa. Lakini alituumba tofauti: Weupe, Weusi, Wanjano,watawala na watawaliwa. Katika upeo sisi ni bora kuliko watu weusi na hilo halina ubishi.

*MITANDAO*



## Kongwa waonyeshwa fursa mkonge, korosho

**Na Augusta Njoji,** KONGWA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, amewataka wakulima wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma kuanzisha mashamba ya korosho na mkonge kutokana na kuhimili ukame.

Kusaya alitoa rai hiyo jana alipotembelea kijiji cha Makutani wilayani Kongwa kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la korosho waliloanza kulima mwaka 2018.

Alisema mazao hayo yanastawi na kuvumilia hali ya ukame hali itakayosaidia kuwa na mazao ya biashara ya kudumu yatakayowapatia kipato cha uhakika.

Akizungumzia kuhusu korosho, Katibu Mkuu huyo alisema katika msimu wa mwaka 2019/20 miche 303,095 ya korosho bora iligawiwa na kupandwa na wakulima wapatao 386 wa wilaya hiyo.

Alisema mwaka 2020/21 jumla ya kilo 3,000 (tani 3) za mbegu bora ya korosho imeagizwa kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Naliendele ili igawiwe kwa wakulima, vikundi na taasisi.

"Pamoja na korosho wakulima wa Kongwa limeni mkonge kwa kuwa unavumilia hali ya hewa ya ukame. Ukipanda leo mkonge baada ya miaka mitatu utaanza kuvuna na kuendelea hadi baada ya miaka 15," alisema.

Kuhusu mkonge, Kusaya alisema zao hilo sasa linalimwa kwenye mikoa 17 ya Tanzania Bara ikiwamo Dodoma.

"Wizara ipo tayari kuleta wataalamu wa mazao haya Kongwa kuwafundisha maofisa ugani kilimo bora na chenye kulenga kuongeza uzalishaji ili wawasaidie wakulima vijijini," alisema.

Awali, Kusaya alitembelea shamba la korosho la mkulima Berling Sospeter wa kijiji cha Makutani lenye ukubwa wa ekari 325 na kumpongeza kwa kilimo hicho.

Akizungumza mkulima huyo, alisema kuna tatizo la upatikanaji wa dawa ya kupulizia mikorosho na kuiomba wizara ichukue hatua kudhibiti uwepo wa dawa zisizo na ubora.

Katika hatua nyingine, Kusaya alikabidhi pikipiki tatu zenye thamani ya Sh. milioni 15 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa Dk.Omary Mkulo, ili ziwasaidie maofisa ugani kuwafikia wakulima vijijini.

"Hizi pikipiki zitumike na maofisa ugani kusimamia uanzishwaji mashamba ya korosho na mkonge nataka maofisa kilimo wasikae ofisini waende vijijini kuhudumia wakulima kuongeza uzalishaji," alisema Kusaya.

Akizungumza kwenye ziara hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri, Dk. Mkulo alisema wamepanga kuzalisha miche bora ya korosho 420,000 na kuigawa kwa kata zote 22, ili wakulima wengi walime zao hilo la biashara.

"Halmashauri ya Kongwa kuna maofisa ugani 58 lakini wote hawana usafiri wa kuwasaidia kuwatembelea wakulima, tunaomba wizara itusaidie pikipiki zaidi ya hizi tatu ili zitumike kuhamasisha kilimo," aliomba.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Suleiman Serera, alisema wakulima wana utayari wa kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara ikiwamo korosho, mkonge na karanga, lakini wanakosa wataalamu wa kuwafundisha kwa karibu.

# Ahadi saba za Mavunde Jimbo la Dodoma Mjini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Dodoma Mjini kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Anthony Mavunde, ametoa ahadi saba kwa wananchi wa jimbo hilo ikiwamo kuchimba visima vikubwa vitano vya maji ili kuondoa kero ya maji.

Mavunde alitoa ahadi hizo juzi katika mkutano wake wa kampeni uliofanyika Kata ya Nala, jijini hapa.

Alisema endapo wananchi wakimpa ridhaa tena ya kuongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo atahakikisha anatatua kero ya maji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DUWASA) kwa kuchimba visima katika Kata ya Zuzu, ili visambaze maji katika eneo la Nala, Mahungu, Zuzu na Nkuhungu.

**Pia nawaahidi nitashughulikia malipo ya fidia ya wananchi wanaopisha ujenzi wa barabara pete (ring road).**

Aidha, aliahidi ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Kata ya Nala ambapo tayari eneo la ekari 33 limetengwa.

"Miaka mitano mliyonipa ilikuwa ya kujifunza na nimeahidi na kutekeleza, naomba mnichague tena kukamilisha usambazaji wa umeme katika maeneo yaliyobakia kupitia programu ya ujaziliaji (densification)," alisema.

Pia, alisema atahakikisha anafungua barabara katika viwanja vipya vilivyopimwa. Aliahidi kujenga shule za msingi mpya katika eneo la Segu na Nala.

"Pia nawaahidi nitashughulikia malipo ya fidia ya wananchi wanaopisha ujenzi wa barabara pete (ring road) na kushughulikia migogoro ya ardhi," alisema.



Mafundi wakiwa katika ujenzi wa mitaro ya maji katika Barabara ya Dodoma - Arusha, eneo la Mailimbili, jijini Dodoma jana. Eneo hilo, limekuwa na changamoto ya kujaa maji wakati wa msimu wa mvua na kusababisha barabara hiyo kuharibika. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanufaika TASAF wapewa mbinu

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

WANUFAIKA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wametakiwa kuzitumia fedha hizo wanazopata kuanzisha miradi ili kujikwamua kiuchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kongwa, Dk. Omary Mkulo, aliyasema hayo juzi alipotembelea baadhi ya kaya maskini ambazo zimehakikiwa upya kwenye mpango huo.

Alisema miradi watakayoanzisha itaongeza kipato cha familia na kuondokana na umaskini.

"Huu mpango umekuwa wa muda mrefu, lakini tusiwe watu wa kupokea na kutumia vibaya, hakikisheni unazitumia fedha hizo kwa kuanzisha miradi ili kuondoka huko kwenye umaskini," alisema.

Aliitaja miradi ambayo wahusika waanzishe ni ufugaji wa kuku na ng'ombe, kilimo cha mazao ya biashara na chakula pamoja na kuanzisha vibanda na maduka ya biashara.

"Kuna biashara zingine sio lazima ufungue duka kubwa, tengeneza meza ukawa unauza biashara yako ya nyanya au vitunguu na hakuna wa kukudai kodi ya pango," alisema.

Aliwataka kujenga uaminifu katika familia zao kwa kushirikiana kupanga matumizi ya fedha wanazopokea.

Alibainisha kuwa serikali inatoa fedha hizo kwa malengo ya kuwaondoa umaskini na kuwa na uhakika wa chakula.

Aidha, alisema jumla ya kaya 6,897 zilihakikiwa kati ya kaya 7,821 zilizopangwa kuhakikiwa sawa na asilimia 88.

"Kaya 924 hazikuhakikiwa kutokana na wahusika kutokuwapo wakati wa uhakiki uliofanyika kwenye vijiji 43 vya wilaya hiyo," alisema.





# Wakosa mikopo elimu ya juu

Na Nebart Msokwa, MBEYA

BAADHI ya watoto yatima ambao wamefaulu mitihani ya kidato cha sita na kuchaguliwa kujiunga na vyuo vikuu, wameshindwa kujiunga na vyuo hivyo baada ya kukosa mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HELSEB).

Msimamizi wa Kituo cha Kulelea Watoto Yatima cha Mkate, Iwambi jijini Mbeya, kinachomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde, Sabina Siwale, aliyasema hayo juzi wakati baadhi ya wadau walipofika kituoni hapo kutoa misaada ya kibinadamu.

Alisema katika kituo hicho kuna watoto wawili ambao wamedahiliwa kujiunga vyuo vikuu, lakini hawawezi kwenda masomoni kutokana na kukosa uwezo wa kugharimia ada na gharama zingine zinazohitajika.

**Vituo vya kulelea yatima vinasaidia kupunguza tatizo la watoto wa mitaani kwa kuwakusanya na kuwalea, jukumu ambalo linapaswa kubebwa na jamii nzima.**

"Katika kituo chetu tunao watoto wawili ambao tulikuwa tukiwasomesha na wamefaulu vizuri mtihani wa kidato cha sita, waliomba mkopo HESLB, lakini hawajapata hivyo hawana uhakika wa kuendelea na masomo yao," alisema Siwale.

Alisema katika kituo hicho wako wanafunzi wengine ambao wanasoma vyuo vikuu waliopata mikopo kwa kiwango kidogo, hivyo kituo kina jukumu la kuwaongezea fedha hali ambayo inadhoofisha uwezo wa kituo kuendelea kugharimia wanafunzi wengine zaidi.

"Tunao wanafunzi 29 tunaowasomesha katika hatua mbalimbali za kielimu, wako walioko sekondari na wengine wanasoma vyuo vikuu. Wote hawa kituo hiki kinawagharamia mahitaji yao. Kwa wale wa vyuo vikuu, baadhi yao wamepata mikopo kwa kiwango kidogo, hivyo tunalazimika kuwaongezea fedha ili kukidhi mahitaji yao," alisema Siwale.

Baadhi ya wadau waliofika kituoni hapo kuwapatia watoto mahitaji ya kibinadamu walisema kuna umuhimu wa jamii kusaidia vituo vya kulelea yatima kuhakikisha watoto wanapata mahitaji yao yote ikiwamo ya kielimu kutokana na umuhimu wa vituo hivyo kwenye jamii.

Steven Upamba, mmoja wa wadau hao, alisema vituo vya kulelea yatima vinasaidia kupunguza tatizo la watoto wa mitaani kwa kuwakusanya na kuwalea, jukumu ambalo linapaswa kubebwa na jamii nzima.

Alisema ikiwa jamii nzima itawajibika kusaidia upatikanaji wa mahitaji ya watoto itasababisha vituo hivyo kuwa na uwezo na nguvu ya kuwakusanya watoto wengi zaidi waliozagaa mitaani na hatimaye kumaliza kabisa kero ya uwepo wa watoto wa mitaani.

Baadhi ya watoto wa kituo hicho waliwashukuru wadau hao kwa kuwapatia misaada ya kibinadamu ambayo ni mahitaji yao ya kila siku kama vile chakula, mafuta, chumvi na sabuni.



Wachuuzi wa matunda wakisubiri wateja katika kituo kikuu cha mabasi cha Mkoa wa Mbeya juzi, shughuli inayowapatia ujira wa siku. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wamtaka mgombea udiwani kutekeleza miradi aliyoianzisha

Na Nebart Msokwa, CHUNYA

WANANCHI wa Kata ya Lualaje katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wamemwomba mgombea udiwani kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Tusalimu Mwaijande, kutekeleza miradi aliyoianzisha katika kipindi kilichopita.

Wananchi hao waliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa kampeni za udiwani za CCM zilizofanyika katika kata hiyo na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa chama hicho wa kata na wilaya.

Mmoja wa wananchi hao, Juma Ramadhan, alisema mgombea udiwani huyo aliiongoza kata hiyo vipindi viwili kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka huu na kuna miradi aliianzisha, lakini mpaka sasa baadhi haijakamilika.

Alisema kutokana na utendaji kazi wa diwani huyo, wanataka akichaguliwa ahakikishe anatekeleza miradi hiyo iliyobakia kwa maelezo kuwa kata hiyo ina matatizo mengi ambayo yanahitaji kutatuliwa ili wananchi wafanye kazi za maendeleo kwa uhuru.

"Katika kata hii kuna matatizo mengi, hivyo tunataka diwani huyu arudi ili aweze kukamilisha miradi aliyoianzisha, tunaamini kuwa usumbufu tulioupata kwa muda mrefu utaisha kabisa," alisema Ramadhan.

Mgombea huyo alisema amefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali hivyo wananchi wakimchagua tena atahakikisha anakamilisha miradi iliyobaki.

Mwaijande alisema katika kipindi kilichopita alisimamia miradi mbalimbali ambayo ni ujenzi wa madaraja mawili, kituo cha afya, ujenzi wa zahanati na ujenzi wa madarasa yaliyokuwa yakiwasumbua wananchi.

# Madereva bajaji wakumbushwa sheria

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

MADEREVA wa bajaji katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wamekumbushwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ili kuepusha ajali za barabarani na matukio mengine yanayoghharimu maisha ya watu.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alitoa kauli hiyo jana kwenye kikao kilichowahusisha madereva na wamiliki wa bajaji, Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) na Jeshi la Polisi kwa lengo la kujadili vikwazo wanavyokumbana navyo waendesha bajaji na vitendo vya uhalifu.

Matei alisema bajaji zinaweza kuchangia vitendo vya uhalifu kwa sababu zinabeba watu wa aina mbalimbali, hivyo madereva wanapaswa kuwa makini kwa kuhakikisha wanapohisi watu wasio wa kawaida watoe, taarifa kwenye vyombo vya usalama.

Alisema kipindi hiki cha uchaguzi kinahitaji umakini mkubwa kwa kuwa watu wanaweza kufanya uhalifu au madhara kwa wengine kwa kutumia usafiri huo wa bajaji.

"Nawakumbusha madereva wote kuzingatia kanuni, sheria na taratibu za usalama barabarani kwa kuhakikisha wanaepuka ajali na matukio ya uhalifu. Lakini kipindi hiki cha uchaguzi nawaomba msiwe sehemu ya kuleta migogoro na vitendo vya uvunjifu wa amani msikubali kutumiwa kwa mambo ya hivyo na wanasiasa," alisema Matei.

Mwenyekiti wa Madereva wa Bajaji wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Iddi Kasangula, alisema madereva wengi wa bajaji wamekuwa wakikamatwa na TARURA kwa madai kuwa wanaegesha kwenye maeneo yaliyopigwa marufuku sambamba na kudaiwa kutolipa ushuru.

Kuhusu uhalifu, Kasangula alisema mara nyingi hufanyika majira ya usiku ambapo baadhi ya madereva ambao wengi ni (deiwaka) hubeba wahalifu kwa kutokujua au wengine hushirikiana nao kutekeleza vitendo hivyo.

Kutokana na sababu hizo, aliahidi kushirikiana na Jeshi la Polisi kuripoti vitendo hivyo pamoja na kuwaambia madereva wote kutofumbia matukio hayo pindi wanapoyaona.

Mwakilishi wa TARURA jijini Mbeya, Akalu Nyari, alisema suala la ushuru ni la kizalendo kwa sababu kupitia fedha hizo, maendeleo yanapatikana ndani ya jamii ikiwamo ujenzi wa shule, hospitali na maji.

Kwa mantiki hiyo, alisema madereva wa bajaji wataendelea kulipa ushuru na kuongeza kuwa suala la kukamatwa kwa bajaji zinazopaki kwenye maeneo yaliyopigwa marufuku litaendelea ili liwe fundisho kwa wengine.

# Balozi Iddi awapa somo wahandisi miradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amewataka wahandisi wanaopewa miradi ya ujenzi, kuhakikisha wanazingatia ubora wa miundombinu wanayoisimamia ili kuepuka hasara au maafa.

Balozi Iddi alisema hayo jana wakati akizungumza na uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na wahandisi wa ujenzi wa msingi wa kupitishia maji ya mvua katika eneo la Mfenesini, Unguja alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo.

Alisema ipo miradi tofauti inayoanzishwa kwa nia ya kuwaondolea shida na usumbufu wananchi, lakini matokeo yake ndani ya muda mfupi baadhi ya miradi huleta athari na kutokidhi mahitaji halisi kutokana na kukosa kiwango kinachokusudiwa kitaalamu.

**Mfenesini ni moja ya maeneo yanayokumbwa na mafuriko wakati wa masika hali hiyo imeongezeka mwaka huu kutokana na mradi wa ujenzi mkubwa wa barabara ya Bububu hadi Mkokotoni.**

Makamu wa Rais aliwataka wahandisi wa ujenzi wa mradi huo kutafuta mbinu za ziada katika kuona changamoto inayowakabili wananchi wa eneo hilo ya kufurika kwa maji ya mvua hasa wakati wa masika inaondoka au kupungua.

Alisema Mfenesini ni moja ya maeneo yanayokumbwa na mafuriko wakati wa masika hali hiyo imeongezeka mwaka huu kutokana na mradi wa ujenzi mkubwa wa barabara ya Bububu hadi Mkokotoni.

Balozi Iddi aliwapongeza wahandisi wa Wizara ya Ujenzi na wale wa kampuni za kimataifa kwa jitihada wanazoendelea kuzichukua kuimarisha miundombinu ambayo imesaidia kuleta ukombozi na ustawi wa jamii.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mustafa Aboud Jumbe, alisema mradi huo wenye urefu wa mita 425 unatarajiwa kumwaga maji ya mvua katika eneo la bondeni.

Alisema wahandisi wamelazimika kubadilisha mfumo wa bomba ili kutoa fursa ya mtiririko wa kasi ya maji ya mvua kwa lengo la kuepuka kutuama kwa mchanga kunakosababisha maji kuanza kusambaa maeneo ya mitaani.

Jumbe alisema maji ni adui mkubwa wa barabara, hivyo lazima uwepo utaratibu mwafaka wa kuhakikisha yanapatiwa njia ya kupita bila ya kuathiri upande wowote.

Eneo la Mfenesini limekuwa na tatizo la kufurika kwa maji ya mvua wakati wa masika na mwaka huu, familia nyingi ziliyahama na kuyaacha makazi yao kutokana na ongezeko kubwa la mvua hizo zilizoleta athari kubwa ya mali zao.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar, Mustafa Aboud Jumbe (wa pili kulia), alipotembelea kukagua ujenzi wa bomba la kupitisha maji ya mvua linalojengwa katika eneo la Mfenesini Meli Kumi, litakalosaidia kupunguza mafuriko ya maji ya mavua mjini Zanzibar jana. **PICHA: OMPR – ZNZ**

## Utawala bora chanzo kupanda kwa uchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUPANDA kwa uchumi nchini kumesababishwa na kuzingatia utawala bora na maadili ya uongozi, imeelezwa.

Sambamba na hayo, mageuzi ya uchumi, utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya jamii na uwekezaji kuendeleza rasilimali watu, vimesaidia kupanda kwa uchumi wa nchi.

Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Ramia Abdiwawa, aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa tawi jipya la Benki ya Diamond Trust (DTB) huko Kijangwani, Zanzibar huku akieleza umuhimu wa kuendeleza jitihada za uchumi jumuishi kutokana na uchumi wa Tanzania kupangwa katika uchumi wa kati na Benki ya Dunia.

Kutokana na hali hiyo, Balozi Ramia aliwataka Wazanzibari kutumia huduma zinazotolewa na benki hiyo katika biashara ndogo (SME) na kushiriki katika uchumi wa daraja la kati (middle class economy).

Waziri huyo aliipongeza benki hiyo kwa kufungua tawi hilo na kusogeza huduma za kifedha karibu na wananchi.

"Najua DTB inatilia mkazo biashara ndogo ambayo inaendesha uchumi, inatoa ajira kwa vijana na kuongeza mapato kwa serikali kupitia ushuru na ubadilishaji wa fedha za kigeni.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa DTB, Viju Cherian, alisema kufunguliwa kwa tawi hilo ambalo ni la pili kwa Zanzibar ni uthibitisho wa ahadi yao kupanua na kupeleka huduma karibu na wananchi ambao hawajajumuishwa katika mfumo wa kifedha.

Alisema benki hiyo imeshiriki katika kujenga uchumi wa Zanzibar kupitia mikopo iliyotolewa kwa wafanyabiashara wadogo hasa katika utalii na uzalishaji.

"Benki pia imetoa zaidi ya Sh. bilioni 100 kwa wafanyabiashara wa Zanzibar tokea kufunguliwa kwa tawi la kwanza miaka 11 iliyopita," alisema.

# Waziri Pembe ataja siri ongezeko ufaulu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amesema uhusiano mzuri kati ya walimu, wazazi na wanafunzi, umesaidia kukuza kiwango cha ufaulu wa daraja la kwanza nchini.

Akizungumza katika kikao cha pamoja baina ya uongozi wa wizara na wakuu wa shule za sekondari za mkoa wa Mjini Magharibi katika ukumbi wa wizara hiyo, Mazizini, alisema ili jamii ifikie malengo ya taifa ya kuzalisha wataalamu wazalendo iko haja ya kuwa na ushirikiano wa karibu miongoni mwao.

Waziri alisema muda umefika kwa jamii kubadilika na kuamini kuwa lengo la kutokomeza alama ya zero na kuondosha kiwango cha ufaulu daraja la nne si la wizara pekee bali linamhusu kila mtu kwa nafasi yake.

Aliwapongeza wakuu hao kwa kupambana na tatizo la utoro kwa wanafunzi shule zao na kwamba hali hiyo pia ni sababu ya kuinua kiwango cha ufaulu.

Pia aliwataka walimu hao kufanya vikao vya karibu baina ya shule moja na shule nyingine bila kubagua shule za serikali au binafsi kujadiliana njia mbadala za kurudisha hadhi ya Zanzibar ya kuzalisha wasomi wa fani mbalimbali.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Idrisa Muslim Hija, alisema serikali ya Zanzibar imepiga hatua kubwa ya kuwa na miundombinu bora ya majengo ya kisasa, hivyo ni jukumu la wazazi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha wanafunzi wanapata matokeo ya daraja la juu.

Aidha, aliwataka wakuu wa shule zenye mchepuo wa michezo kuacha mara moja tabia ya kuwanyanyasa wanaosomesha michezo na masomo hayo yamewekwa kwa lengo la kukuza vibaji vya wanafunzi na faida kwa nchi.

Kuwapo kwa mchepuo wa michezo, alisema ni moja kati ya fani ambazo zinaipa nchi sifa nzuri endapo nchi itazalisha wanamichezo wazuri.

Naye Naibu Katibu Mkuu Utawala na Uendeshaji wa Wizara hiyo, Abdullah Mzee Abdullah, aliwasisitiza walimu na wanafunzi kuzitunza shule za kisasa zilizojengwa ili kizazi kijacho kitumie miundombinu hiyo ikiwa katika ubora.

Wakuu wa shule walioshiriki katika kikao hicho, waliiomba wizara kuanzisha mabweni ya wanafunzi wa kidato cha nne na cha sita yatakayowasaidia wanafunzi kuwa karibu na walimu wao na kupata ufaulu wa juu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kiwanja cha Biashara kinauzwa Regent Estate Dsm mita za mraba 1300. Piga; 0693 689996, 0757 129546.

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

**AMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;264/2020**

**Ombi la JOHN SYLVESTER NGUMA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SYLVESTER JOHN NGUMA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 08/09/2020.

Tarehe 8/9/2020

Sahihi ya Hakimu

115890902

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO TAWA.**

**WILAYA YA MOROGORO.**
**WITO**
**Kwa SAMWERI HAJI.**

Unaamriwa na JAMUHURI uhudhulie katika mahakama hii siku ya ALHAMISI Tarehe 10/09/2020 saa 2:00 Asubuhi ili kujibu

**MADAI 2/2020 - TALAKA.**

**KUITWA SHAURINI HII IMETOLEWA KWA MAOMBI YA:**
**MARIA ADAM**

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 06/08/2020.

MAHAKAMA YA MWANZO TAWA MOROGORO

115891102

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MVUHA.**

**WILAYA YA MOROGORO.**
**WITO**
**Kwa BENNY NJIKU.**

Unaamriwa na JAMUHURI uhudhulie katika mahakama hii siku ya ALHAMISI Tarehe 10/09/2020 saa 2:30 Asubuhi ili kujibu shitaka la **NDOA NA TALAKA.**

**KUITWA SHAURINI HII IMETOLEWA KWA MAOMBI YA:**
**SALOME MWITUMBA**

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 05/08/2020.

MAHAKAMA YA MWANZO MVUHA MOROGORO

115891002

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PHILIPO JONAS MWINGIRA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 887 CJJ.** YENYE CHASSIS NO. **ADAPAJOBYKGB06112.** ENGINE **NO. 129-119-640.** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **MUH/RB/4118/1019.**

115891402

## KUPOTEA KWA CHETI



**AMOSI LUZIGAMA BAHINGAI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0739/0104** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **HIJRA SEMINARY** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/625870/2020.**

115888202

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**TANZANIA CHINA TRADE & TOURISM DEVELOPMENT LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA FEKON YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 688 AAY.** YENYE CHASSIS NO. **LDAPAJOBIEGB20091.** ENGINE NO. **157FM121420091.** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **TAN/RB/566039/2020.**

115891502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 111/2020**

**Ombi la 1. MGENI KIBONGE KHALFAN**
**2. JOHN JOHN CHELELE kuteuliwa**

**Msimamizi wa mirathi Marehemu HIDAYA KHALFAN KIBONGE**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 11/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 01/9/2020

Sahihi ya Hakimu COURT URBAN DODOMA

115891702

**TEGEMEZA FINANCE AND COURT BROKER LTD**
**P.O. Box 77593, DAR ES SALAAM. SIMU: 0719 187677.**

## TANGAZO LA MNADA NA NOTISI

Kwa idhini tuliyopewa na Mahakama ya Mwanzo Buguruni tunawatangazia watu wote kutakuwa na mnada wa hadhara tarehe **19/9/2020** saa **4:00 asubuhi** eneo la **Mbezi Beach Bondeni.** Aina ya bidhaa ni gari aina ya **IST yenye namba T 151 DRA itauzwa.**

**TARATIBU ZA MNADA**

1. Mteja atalipa 25% siku ya mnada
2. Awamu ya pili ndani ya siku 14 awe amemaliza 75%
3. Kama mteja atashindwa kumaliza deni ndani ya siku 14 hela haitarudishwa iliyotolewa awali.
4. Mali itauzwa kama jinsi ilivyo, pia mali hatapewa mteja mpaka awe amefanya malipo yote.
5. Mteja anaruhusiwa kuja kukagua mali inayouzwa kabla ya siku ya mnada.

115891602

Uza,

Chenye Thamani

Kubwa Kwa Kutangaza

Nasi Kwa Bei Poa

Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Madai ya watumishi kuratibiwa kimtandao

**Na Gideon Mwanosya,** SONGEA

SERIKALI imeanza kuratibu madai na madeni ya watumishi yasiyo ya mishahara kwa njia ya kielektroniki.

Mwezeshaji wa mafunzo ya mfumo wa madeni (MADENI MIS) kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Nestory Mgimwa, ndiye aliyebainisha hayo alipokuwa akitoa mafunzo kwa wakuu wa idara na vitengo katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma.

Mgimwa alisema kwamba kundi la kwanza kunufaika na mfumo huo ni walimu, na kuwa serikali imeanza kuratibu madeni hayo kwa lengo la kuyatambua na kuyaingiza kwenye MADENI MIS, lengo ni kupata takwimu sahihi za madeni halali ya watumishi na kukabiliana na udanganyifu wa madeni hewa.

Alizitaja faida za mfumo huo kuwa ni kuongeza uwazi, uwajibikaji, ari ya kufanya kazi na kuondoa usumbufu pamoja na gharama kwa watumishi wanapokuwa wanakifuatilia stahiki za madeni yao.

"Wanufaika wa kwanza kwenye mfumo huu ni walimu ambao ni asilimia 52 kati ya watumishi wote wa halmashauri nchini," alifafanua Mgimwa.

Hata hivyo alisema watumishi katika mfumo huu wanatakiwa kutoa taarifa za ukweli na sahihi katika kudai madai yao kwa kuwasilisha viambatanisho stahiki, na kwamba ni kosa la kisheria kughushi nyaraka kwa lengo la kujipatia malipo.


NOTICE FOR CONVENING OF THE 22ND NATIONAL GENERAL CONVENTION

The President of the Media Council of Tanzania (MCT), does hereby pursuant to Article 13 of the MCT Constitution give notice to members of MCT that the 22nd National General Convention (NGC) of the Media Council of Tanzania (MCT) shall be held on September 28, 2020 at Tanga Beach Resort in Tanga.

PROPOSED AGENDA

1. Opening;
2. Adoption of Agenda;
3. Minutes of the 21st National General Convention held at Seashells Hotel in Dar es Salaam on November 19, 2019;
4. Matters arising from the 21st NGC;
5. Report of the Executive Secretary;
6. Adoption of 2019 Audited Financial Statements;
7. Appointment of External Auditors for the period ending December 31, 2020;
8. Adoption of 2020 reviewed Code of Ethics;
9. Election of Governing Board;
10. A.O.B;
11. Closing

MCT members who have not paid their annual subscription fees during the prescribed time are hereby reminded to do so promptly.

Judge Thomas B. Mihayo
President
Media Council of Tanzania (MCT)




Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, Vivianne Penessis, akizungumza na sehemu ya wanafunzi 60 wa shule mbalimbali za sekondari, wakati wa kuhitimu mafunzo ya kuwajengea uwezo wasichana katika masomo ya sayansi, yaliyoandaliwa na Tanzania Data Lab, kwa udhamini wa kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtandao wa elimu waishauri wizara kukabiliana na majanga

**Na Elizabeth Zaya**

MTANDAO wa Elimu Tanzania (TENMET), umeiomba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuja na mbinu mbadala za kiteknolojia ambazo zitakuwa zinatumika katika vipindi vya majanga kuepusha athari za kielimu.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Saalam na Mratibu wa TENMET, Ochola Wayoga, wakati akizungumza na waandishi wa habari ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Ulinzi wa Elimu dhidi ya mashambulio ambayo hufanyika Septemba 9, kila mwaka duniani.

Alisema janga la corona linapaswa kutumika kujifunzia umuhimu wa kuwa na mifumo mbadala ya kiteknolojia ambayo itasaidia shughuli za elimu kuendelea hata kunapotokea majanga badala ya kusitisha shughuli hizo.

"Serikali itumie COVID-19 kama somo la kuinua utoaji wa elimu kwa njia ya teknolojia ili hata ikitokea majanga, kufundisha na kujifunza kusiathirike kwa kiasi kikubwa kama ilivyotokea mwaka huu," alisema Wayoga.

Pia aliiomba Wizara hiyo ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kufanya tathmini itakayolenga kubaini hatari za kuathiri ufundishaji na ujifunzaji katika sekta hiyo ya elimu kipindi cha majanga kama ilivyotokea kipindi cha ugonjwa wa corona.

Jingine aliiomba kuweka mikakati ya kuzuia na kuzihakikishia shule zote usalama kwa kupitia na kufuatilia maelekezo ya Wakala wa Afya na Usalama Mahala pa Kazi (OSHA).

"Ulinzi wa elimu dhidi ya majanga ni jukumu letu sote kama Watanzania na wadau wa elimu ili kufikia maendeleo endelevu ya dunia 2030 na dira ya maendeleo ya taifa ya mwaka 2025," alisema Wayoga.

Wayoga alisema sekta hiyo ya elimu imekuwa ikiingiliwa na mashambulizi ambayo huathiri kufundisha na kujifunza kusifanikiwe kama inavyotarajiwa.

Alitaja mambo mengine ambayo yamekuwa yakileta mashambulizi na athari katika sekta ya elimu kuwa ni pamoja na wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda na kutoka shuleni na hata kusababisha utoro.


NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **RIMBO COMPANY LIMITED, WAUNGWANA AUCTION MART na GADAU AUCTION MART & COMPANY LIMITED** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili, Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TEMEKE | RIMBO COMPANY LIMITED | MWAIJIBE/W,SIKITU | MWAIJIBE/W,SIKITU | KIWANJA | KISARAWE - KIGAMBONI | 23/09/2020 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI |
| 2 | TEMEKE | RIMBO COMPANY LIMITED | ISHEMBE/R,SILIVESTER | MABERE/MAUGO,FAIDA | KIWANJA | KISARAWE - KIGAMBONI | 23/09/2020 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI |
| 3 | TEMEKE | RIMBO COMPANY LIMITED | YANGWIKE/RASHIDI,FATUMA | KIMO/KASSIMU,MALIKI | NYUMBA | MBAGALA - NZASA | 24/09/2020 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI |
| 4. | TEMEKE | RIMBO COMPANY LIMITED | MOHAMED/O,ISMAILI | MOHAMED/O,ISMAILI | KIWANJA | KILONGONI - KAZOLE | 24/09/2020 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI |
| 5. | TEMEKE | RIMBO COMPANY LIMITED | MSELEM/AHMADI,FATUMA | MSELEM/AHMADI,FATUMA | NYUMBA | KISEMVULE | 25/09/2020 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI |
| 6 | TEMEKE | GADAU AUCTION MART & COMPANY LIMITED | MBUGITA/M,YOTHAM | MBUGITA/M,YOTHAM | NYUMBA | KISEWE - MBANDE | 23/09/2020 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI |
| 7 | TEMEKE | RIMBO COMPANY LIMITED | KYEBITAMA/SAIDI,RUKIA | KYEBITAMA/SAIDI,RUKIA | KIWANJA | MPONDA MBAGALA | 25/09/2020 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI |
| 8 | TEMEKE | RIMBO COMPANY LIMITED | SALUM/ABDUL,SOPHIA | MKUMBA/HAMADI,SAIDI | NYUMBA | CHAMAZI KANISANI | 26/09/2020 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI |
| 9 | TEMEKE | RIMBO COMPANY LIMITED | KACHITE/RAMADHANI,SABILI | KACHITE/RAMADHANI,SABILI | KIWANJA | CHAMAZI | 26/09/2020 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI |
| 10 | TEMEKE | RIMBO COMPANY LIMITED | MGENI/JOHN,EDNA | MGENI/JOHN,EDNA | NYUMBA | MAJIMATITU MBAGALA | 26/09/2020 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI |
| 11 | LUMUMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | OLUODO/FANUEL,FURAHA | OLUODO/FANUEL,FURAHA | PAGALE | MIVUMONI | 24/09/2020 SAA 10:00 ASUBUHI |
| 12 | TEMEKE | WAUNGWANA AUCTION MART | MWELELI/FELIX,EUTROPIA | MWELELI/FELIX,EUTROPIA | NYUMBA | PUGU BANGULO | 24/09/2020 SAA 10:00 ASUBUHI |
| 13. | TEMEKE | WAUNGWANA AUCTION MART | MATAU/LEONS,EPAPHRAS | MATAU/LEONS,EPAPHRAS | NYUMBA | KIGILAGILA | 24/09/2020 SAA 10:00 ASUBUHI |
| 14. | TEMEKE | WAUNGWANA AUCTION MART | SADALA/S,MZELELA | SADALA/S,MZELELA | KIWANJA | MALELA MKURANGA | 25/09/2020 SAA 10:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA UKISHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

KWA MAWASILIANO ZAIDI
RIMBO COMPANY LIMITED 0712848820
GADAU AUCTION MART & COMPANY LIMITED 0719813030
WAUNGWANA AUCTION MART 0713077474
WOTE MNAKARIBISHWA.

HABARI MICHEZO




# DEPAY HAJUI KAMA ATAKWENDA BARCELONA

**AMSTERDAM,** Uholanzi

NYOTA wa Lyon, Memphis Depay anajua kwamba huduma yake inatakiwa sehemu nyingine huku akiwa anahusishwa na Barcelona, lakini mshambuliaji huyo hana uhakika kama uhamisho huo utafanikiwa.

Depay amekuwa akiwaniwa na Barca, ambako kocha wa zamani wa Uholanzi, Ronald Koeman amechukua mikoba na pia AS Roma inamwania.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 anajua kwamba anatakiwa, lakini amesema anasubiri kuona kama uhamisho wake utawezekana.

"Tunatakiwa kusubiri kuona kama itatokea. Nitaripoti kwenye klabu ya Lyon kesho (jana) Jumanne," amesema Depay akiiambia NOS baada ya Uholanzi kuchapwa bao 1-0 na Italia kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA.

"Halafu tutaona. Sijasikia zaidi hadi sasa kutoka kwa wakala wangu.

"Najua kuna sehemu natakiwa, lakini sina la zaidi la kusema kwa sababu sijui mambo mengi."

Depay alifunga mabao 15 katika mechi 22 kwa Lyon msimu uliopita licha ya kukaa nje kwa muda mrefu kutokana na majeruhi aliyoyapata Desemba.

Alianza msimu mpya wa 2020-21 kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, kwa kufunga 'hat-trick' dhidi ya Dijon.



# Van Dijk: Uholanzi ilistahili kufungwa

**AMSTERDAM,** Uholanzi

VIRGIL van Dijk anahisi Uholanzi waliadhibiwa kwa kucheza chini ya kiwango wakati wakifungwa na Italia 1-0 kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Bao la kichwa la Nicolo Barella liliwahakikishia ushindi Azzurri mjini Amsterdam na kuwapeleka kileleni mwaka kundi A1, wakiongoza kwa pointi moja dhidi ya Oranje hao.

Nahodha, Van Dijk anafikiria kikosi chake kilistahili kufungwa kutokana na kutokuwa kwenye kiwango chao bora.

"Ulikuwa mchezo tuliocheza chini ya kiwango," alisema mlinzi huyo wa Liverpool akiiambia NOS.

"Kwa uhakika hatukuwa kwenye presha kubwa, tulikuwa kwenye kiwango kibovu kabisa.

"Uwanja wa nyumbani haukutusaidia, lakini tulistahili kufungwa. Tunatakiwa kuwa imara na bora kwenye mchezo unaofuata.

"Kipindi cha kwanza hakikuwa kizuri. Baada ya mapumziko tulijaribu kurudi mchezoni, na unaweza kuoa tulijaribu kucheza vizuri, lakini hatukuwa kwenye kiwango kizuri."

# Chiellini bado ni beki bora duniani - Mancini

**AMSTERDAM,** Uholanzi

ROBERTO Mancini amesema Giorgio Chiellini bado anaweza kuwanoa walinzi wengi duniani namna ya kufanya kazi yao baada ya kurudi dimbani kuichezea Timu ya Taifa ya Italia.

Mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 36, Jumatatu alicheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa tangu Juni mwaka 2019, akionyesha kiwango cha kuvutia kwa Azzurri hao ambao walimchapa Uholanzi bao 1-0 kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA mjini Amsterdam.

Chiellini alifanyiwa upasuaji wa mguu Septemba mwaka jana na alicheza mechi nne tu kwa Juventus msimu wa 2019-20.

Mancini hana shaka na umuhimu wa mlinzi huyo wa kati katika mipango yake kwenye kikosi hicho.

"Ana uzoefu wa kutosha, ubora... bado anaweza kuwafundisha walinzi wengine duniani," amesema Mancini kocha wa timu ya taifa ya Italia.

"Ni muhimu kwa upande wetu kuwa nae uwanjani kwa sababu ya ari yake ya kupambana. Nina furaha amerudi na aliweza kucheza bila tatizo lolote."

Chiellini mwenyewe baada ya mchezo huo alikubali kwamba alikuwa na hamu kubwa kuichezea Italia, ambapo alikuwa nje kwa zaidi ya mwaka baada ya kufanyiwa upasuaji.

"Tulijiandaa vizuri kwa mchezo huu na kucheza kwa kiwango cha juu zaidi," alisema Chiellini akiiambia Rai Sport.



## HABARI MICHEZO

# Mbappe akutwa na virusi vya corona

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe amepimwa na kukutwa na virusi vya corona.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 aliondoka kwenye kikosi cha Ufaransa baada ya vipimo kuonyesha kuwa ameambukizwa virusi hivyo kabla ya mchezo wao wa Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya Croatia jana Jumanne.

Mbappe pia anatarajiwa kutokuwapo katika kikosi cha PSG kwenye mechi za Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, dhidi ya Lens, Marseille, Metz na Nice kwani amekwenda kukaa karantini kwa siku 14.

Awali straika huyo wa zamani wa Monaco alitarajiwa kucheza dhidi ya Croatia jana Jumanne, baada ya kuumia kifundo cha mguu wakati wa mchezo wa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Sweden, Jumamosi iliyopita.

"Kylian Mbappe ataukosa mchezo dhidi ya Croatia," ilisema taarifa fupi ya Ufaransa kupitia ukurasa wake wa Twitter Jumatatu.

"Amekutwa na ugonjwa wa COVID-19 – na ameondolewa kikosini haraka ili akakae peke yake kwa kujitenga."

Golikipa, Steve Mandanda na kiungo Houssem Aouar tayari walikuwa wameshaondolewa kwenye kikosi hicho cha Ufaransa baada ya kupatikana pia na virusi vya corona.

Kiungo wa Manchester United, Paul Pogba, alilazimika kujiondoa katika kikosi hicho kabla ya Didier Deschamps kukitangaza kikosi cha mwisho kuelekea mechi hizo za mataifa ya UEFA, baada na yeye kugundulika ana virusi vya corona.

Wakati huo huo, wachezaji sita wa PSG wamethibitishwa kuwa na virusi hivyo na hivyo wamewekwa karantini, lakini majina yao hayajatajwa.

Kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel kinatarajia kuanza kampeni ya kutetea taji lake la Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, dhidi ya Lens Alhamisi hii.

PSG ilicheleweshwa kuanza ligi hiyo iliyoanza wiki iliyopita baada ya kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwezi uliopita.





# MARTIAL KIWANGO CHAKE KIMEIMARIKA - LLORIS

**PARIS,** Ufaransa

GOLIKIPA wa Ufaransa, Hugo Lloris anaamini Anthony Martial amekuwa na kujiamini zaidi chini ya Ole Gunnar Solskjaer pale Manchester United.

Fowadi huyo alicheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa tangu Machi mwaka 2018, wakati alipoingia akitokea benchi kwenye ushindi wa Ufaransa wa 1-0 dhidi ya Sweden kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA, Jumamosi iliyopita.

Martial alipata penalti baada ya kufanyiwa faulo na mchezaji mwenzake wa United, Victor Lindelof na Antoine Griezmann akashindwa kufunga, kabla ya Kylian Mbappe kufunga bao hilo pekee.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amefunga mabao 23 katika mashindano yote katika ngazi ya klabu msimu uliopita.

Lloris anafikiri sasa presha kubwa iko kwa Martial kuhakikisha anakuwa kwenye kiwango bora zaidi, lakini nahodha huyo wa Tottenham anaamini nyota huyo wa zamani wa Monaco atanufaika kucheza chini ya Solskjaer pale United.

"Sijui ana uhusiano gani na Solskjaer, lakini nafikiri anajiamini sana," alisema Lloris.

"Kuna maelewano mazuri kwa wachezaji wanaomzunguka pale Manchester United. Naamini atakuwa na mafanikio mazuri zaidi na kiwango chake kuzidi kuimarika kule."

# *Everton yamsajili rasmi Rodriguez*

**LONDON,** England

JAMES Rodriguez ameondoka Real Madrid na kujiunga na miamba wa Ligi Kuu England, Everton kwa mkataba wa miaka miwili huku kukiwa na kipengele cha kumwongeza mwaka wa tatu.

Akiwa amekosa nafasi chini ya kocha, Zinedine Zidane, James ameungana na Kocha Carlo Ancelotti - ambaye alimnoa wakati akiwa Madrid na Bayern Munich kwa ada iliyoripotiwa ya pauni milioni 20.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 raia wa Colombia alicheza mechi 14 kwa mabingwa hao wa LaLiga msimu uliopita, akifunga bao moja.

Rodriguez amewasili Everton kama usajili wa pili mkubwa katika kipindi hiki cha dirisha kubwa la majira ya joto, baada ya kuwasili kwa Allan kutoka Napoli, ambapo ilithibitishwa Jumamosi.

Ancelotti itatumaini kiungo huyo wa zamani wa Porto na Monaco atakuwa kwenye kiwango chake kama alichokionyesha msimu wake wa kwanza kule Madrid, wakati Everton ikijipanga kuimarika zaidi tofauti na msimu uliopita, ambapo walimaliza nafasi ya 12.

"Kwa hakika, nina furaha kubwa sana kuwa katika klabu kubwa kama hii, klabu yenye historia nyingi na nikiwa hapa na kocha ninayemfahamu na anayenifahamu vizuri," alisema Rogriguez akiambia evertonfc.com.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HATIMAYE MESSI AREJEA BARCA

## Nahodha huyo ameanza mazoezi na wenzake baada ya mpango wa kuondoka...

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi alikuwa sehemu ya mazoezi ya kikosi cha Barcelona juzi Jumatatu, ikiwa ni mara ya kwanza kuonekana na timu hiyo tangu mpango wake wa kutaka kuondoka kushindikana.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alithibitisha Ijumaa iliyopita kwamba, atabakia pale Camp Nou baada ya kushindwa kufanikisha mchakato wa kuondoka klabuni hapo.

Messi aliamini anaweza kutumia kipengele cha mkataba wa kuondoka huru, lakini Barca na LaLiga walibainisha kwamba hataweza kuondoka huru kwa sababu kipengele hicho cha kuondoka kwa euro milioni 700 bado kinafanya kazi.

**Nyota huyo mwenye umri wa miaka 33 alimshutumu Rais wa Barca, Josep Maria Bartomeu kwa kushindwa kutimiza ahadi yake ya kumruhusu kuondoka huru wakati atakapotaka kufanya hivyo, lakini sasa atabakia klabuni hapo kwa msimu wa 2020-21.**

Messi, alipigwa picha akiwasili na gari lake kwenye mazoezi ya klabu hiyo Jumatatu.

Kwa mujibu wa gazeti la Marca, mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or alionekana hapo kwenye uwanja wa Sant Joan Despi kwa mara ya kwanza na aliwasili mapema zaidi, nusu saa kabla ya mazoezi kuanza.

Baadaye Barca iliweka picha ya Messi kwenye ukurasa wake wa Twitter ikimwonyesha Messi akifanya mazoezi na kocha mpya, Ronald Koeman kwa mara ya kwanza.

Miamba hao wa Katalunya wataanza kampeni yao ya Ligi Kuu dhidi ya Villarreal baadaye mwezi huu.

## ZISIKUPITE

### UNITED YASAKA WATATU

MANCHESTER United inaamini itafanikiwa kunasa nyota watatu wapya kabla ya dirisha la usajili halijafungwa na mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (20), akiwa ni mmoja wa wachezaji inaowahitaji. ***(Manchester Evening News)***

### BALE NJIA PANDA

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane ndiye mwenye uamuzi wa mwisho wa kuteua kikosi chake huku Manchester United ikionyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale (31). ***(Marca - in Spanish)***

### TELLES ANUKIA UNITED

WAWAKILISHI wa beki wa kushoto wa Porto, Mbrazili, Alex Telles ambaye ana umri wa miaka 27, wamesafiri kwenda katika Jiji la Manchester kwa ajili ya kufanya mazungumzo na mabosi wa klabu hiyo ya United. ***(A Bola - in Portuguese)***

### CARLOS AKARIBIA CITY

MANCHESTER City imemtaja beki wa Sevilla Mbrazili, Diego Carlos (27), na nyota wa Atletico Madrid ambaye ni raia wa Uruguay, Jose Gimenez (25), kuwa mbadala wa beki wa kati wa Napoli na Timu ya Taifa ya Senegal, Kalidou Koulibaly (29). ***(Sport - in Spanish)***

### KING ATAJWA VILLA

BAADA ya kukosa saini ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Callum Wilson, mabosi wa Aston Villa wamewasilisha ofa ya pauni milioni 16 kwa Bournemouth ili kumsajili straika wa Norway, Josh King (28). ***(Telegraph - subscription required)***

### BREWSTER AINGIA SOKONI

ASTON Villa imeweka wazi inataka kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 21 ya England (U-21), Rhian Brewster akitokea Liverpool kwa ada ya pauni milioni 20. Sheffield United na Crystal Palace zinawania pia saini ya nyota huyo. ***(Telegraph - subscription required)***

### BARCA YAMTAKA ALCANTARA

BARCELONA imeweka wazi inahitaji huduma ya kiungo wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Hispania, Thiago Alcantara (29), ambaye anawania na Liverpool. ***(Bild - in German)***

### TARKOWSKI AITESA WEST

WEST Ham United ambayo iliweka dau la pauni milioni 30, inajiandaa kuongeza fedha ili kumpa beki wa kati wa Burnley na Timu ya Taifa ya England, James Tarkowski. ***(Evening Standard)***

### MENDY KUTUA CHELSEA

CHELSEA imetangaza mpango wake wa kuwania saini ya golikipa wa Rennes na Timu ya Taifa ya Senegal, Edouard Mendy, ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Telegraph - subscription required)***

### WOLVES YAMFUATA FERREIRA

KLABU ya Wolverhampton Wanderers imekaribia kunasa saini ya kiungo wa Porto na Timu ya Taifa ya Ureno, Vitor Ferreira (20), kwa kumpa mkataba wa muda mrefu na kuweka kipengele cha kumnunua baadaye kwa thamani ya pauni milioni 18. ***(Express and Star)***

HABARI MICHEZO

## Mbeya City FC yalia na mabeki

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Mbeya City yenye maskani yake jijini Mbeya, Amri Said, amesema safu yake ya ulinzi ilionyesha udhaifu mkubwa na ndiyo sababu ya kupokea kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa KMC, katika mechi ya raundi ya kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Amri, alisema wachezaji wake hawakuwa katika kiwango kizuri hali iliyosababisha kuruhusu washambuliaji wa KMC kufanya mashabulizi ya mara kwa mara.

Amri alisema mabeki wake hawakuwa makini na walishindwa kuhimili kasi ya wapinzani wao na hivyo anayafanyia kazi ili kutorudia makosa katika mchezo unaofuata.

"Safu yangu ya ulinzi ilipoteza umakini, hakuna chochote walichokifanya katika mchezo huo, hayakuwa matokeo mazuri na hasa ukizingatia huo ulikuwa ni mchezo wa kwanza," alisema beki huyo wa zamani wa Simba.

Mbali na safu ya ulinzi, Amri alisema idara ya kiungo pia ilishindwa kufanya kazi yake ipasavyo na kuahidi hali hiyo haitaonekana kwenye mchezo unaofuata dhidi ya Yanga, ambao utachezwa Jumapili.

Alisema kuondoka kwa mchezaji wake tegemeo, Peter Mapunda hakujawakatisha tamaa na kuongeza wamesajili wachezaji wengine wapya ambao wako tayari kukabiliana na ushindani katika ligi hiyo.

## Beki wa Yanga arejea Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VITA ya usajili wa wachezaji imeendelea kushika kasi katika timu mbalimbali zinazoshiriki katika msimu wa 2020/21 wa Ligi Kuu Zanzibar, huku KVZ ikitangaza kunasa nyota watatu kutoka Tanzania Bara.

KVZ itaiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Katibu Mkuu wa KVZ, Khamis Abdulhamid Hamid, aliwataja wachezaji waliowasajili ili kuimarisha kikosi chao kuwa ni pamoja na Ali Hamad Ali kutoka Yanga, Nassor Saleh Samtata (Ndanda ), Khamis Majid Bakar (Kagera Sugar) na Talib Hamis Makame wa Kipanga.

Hamid alisema lengo la kusajili nyota hao ni kukiongezea nguvu kikosi chao ili kifanye vizuri kwenye Ligi Kuu Zanzibar na mashindano hayo ya kimataifa.

"Tunasajili wachezaji wazuri kwa kufuata mapendekezo ya kocha wetu, aina ya wachezaji anaowahitaji na kuzingatia nafasi zilizokuwa na mapungufu, usajili wetu wa msimu huu unaangalia zaidi michuano ya CAF pamoja na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar," alisema Hamid.

Aliongeza wanajipanga ili kuweka rekodi nzuri katika michuano ya kimataifa kutokana na klabu nyingi za Zanzibar kutolewa mapema kwenye mashindano ya kimataifa.

# KMC YAANZA KUUOTA UBINGWA WA LIGI KUU



**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi mnono katika mechi yake ya kwanza, Kaimu Kocha Mkuu wa KMC, Habib Kondo (pichani), amesema timu yake imejipanga kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21, imeelezwa.

**KMC ilianza msimu kwa ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Mbeya City kutoka jijini Mbeya.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kondo alisema kikosi chake kilifanya maandalizi mazuri na kimedhamiria kuonyesha ushindani kwenye Ligi Kuu msimu huu na si vinginevyo.

Kondo alisema baada ya kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu miwili mfululizo, wachezaji wake wameingia msimu wa tatu wakiwa na uzoefu, hivyo sasa wanachohitaji ni kugombea ubingwa.

"Msimu wa kwanza ulikuwa mzuri sana mpaka tukacheza michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika. Wa pili haukuwa mzuri, kwa sababu tuliponea chupuchupu kushuka daraja, lakini msimu huu wa tatu tumeona yaliyotokea na tayari tumeshakomaa, hivyo lengo letu ni kushindana kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Kondo, ambaye aliwahi kuwa kiungo klabu ya Nyota Nyekundu.

Aliongeza kila mchezaji wa timu hiyo anatakiwa kuongeza bidii ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi, badala ya kusubiri kupambana wakati wa hatua ya lala salama.

"Tumejipanga kumaliza msimu mapema, ukisubiri kusaka pointi katika mechi za mwisho ni hatari, tutaendelea kupambana ili malengo tuliyonayo yatimie," Kondo alisema.

Yalikuwa ni mabao ya Emmanuel Mvuyekule, Hassan Kabunda, Abdul Hillary, na Paul Peter yaliyoifanya timu hiyo kuondoka uwanjani na pointi tatu muhimu na kuweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza kukaa kileleni baada ya mechi za raundi ya kwanza kumalizika.

KMC itaendelea kubakia jijini na mchezo wake unaofuata utakuwa dhidi ya Tanzania Prisons, ambao utachezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Uhuru.



Kiungo wa Azam FC, Salum Aboubakar 'Sureboy' (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Polisi Tanzania, Maulid Nassor katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam juzi. Azam ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## *Azam FC yahitaji mabao zaidi*

**Na Adam Nyangasa,** Tudarco

LICHA ya kupata ushindi bao 1-0 , Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema anahitaji timu yake kupata mabao mengi zaidi katika mechi za Ligi Kuu Tanzaniza Bara msimu huu, ili kujiweka kwenye nafasi nzuri.

Bao pekee la Azam FC lilifungwa na mshambuliaji wa kimataifa kutoka Zambia, Obrey Chirwa dakika ya 44 akimalizia kwa mpira wa kichwa uliopigwa na Prince Dube.

Akizungumza na gazeti hili, Vivier, alisema wachezaji wake walionyesha kiwango kizuri katika kipindi cha kwanza na dakika 45 za mwisho waliruhusu wapinzani wao kutawala mchezo.

Vivier alisema pia alifurahishwa na viwango vilivyoonyeshwa na wachezaji wake wapya waliosajiliwa na anaamini wataisaidia timu hiyo kufanya vizuri msimu huu.

"Wachezji wapya walioanza walikuwa ni Prince Dube, Ayoub Lyanga pamoja na golikipa, David Mapigano, ambao walifanya vizuri, kipindi cha pili tukafanya mabadiliko wakaingia wengine wawili ambao ni Alain Akono na Awesu Awesu, ambao hawakufanya vizuri kama wengine, lakini nina imani mechi zinazofuata watafanya vizuri," alisema Vivier.

Kuhusu maandalizi ya mechi yao inayofuata dhidi ya Coastal Union, kocha huyo alisema itakuwa na ushindani kwa sababu walipoteza mchezo wao wa kwanza.

Aliongeza kuwa wamejiandaa kupambana ili kuendeleza kasi ya ushindi wakiwa kwenye uwanja wao wa nyumbani na kutoruhusu wapinzani wao kuondoka na pointi.

# Michezo

Jumatano Septemba 9, 2020

Nipashe




Messi arejea kazini Barca UKURASA 22



Mshambuliaji wa Yanga, Yacouba Songne (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Tanzania Prisons, Nurdin Chona katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Zlatko asaka pumzi Yanga

**Na Saada Akida**

WATAIMARIKA! Kocha Mkuu wa Yanga, Zlatko Krmpotic, amesema kazi kubwa anayoifanya sasa ni kuhakikisha wachezaji wake wanakuwa na pumzi ya kutosha ili wapate matokeo mazuri katika mechi zinazofuata za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga inatarajia kuwakaribisha Mbeya City Jumapili usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Zlatko aliliambia gazeti hili kuwa mbali na wachezaji kutokuwa 'fiti', lakini pumzi ni tatizo lingine lililosababisha timu hiyo kuambulia sare ya bao 1-1 katika mchezo wao wa kwanza dhidi ya Tanzania Prisons.

"Wachezaji wangu wanajituma na wanafanya vizuri, nimegundua kwamba tatizo lipo kwenye pumzi na imetokana na kutofanya maandalizi ya muda mrefu, bado tuna muda wa kufanya vizuri, makosa yaliyopo tutayafanyia kazi," alisema Zlatko.

Kocha huyo alisema kikosi chake kitashuka dimbani kikiwa tofauti na anaamini wataondoka na matokeo chanya.

"Nina imani kila tunavyoendelea kucheza, kikosi kitakuwa kinaimarika, ninaona pia wachezaji wameanza kuzoeana na kuimarika zaidi," alisema Zlatko.

Alisema hana tatizo na safu yake ya ushambuliaji inayoongozwa Mghana, Michael Saporng ambaye alifunga bao la kusawazisha katika mchezo wao uliopita.

# Simba kuikabili Mtibwa kivingine

**Na Faustine Feliciane**

**Lengo la Sven ni kujihakikishia ushindi mapema katika mechi hiyo itakayochezwa Jumamosi...**

WAKATI ikitarajia kuelekea Morogoro leo, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema kikosi chake kitaingia tofauti katika mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani humo.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Sven, alisema tayari ameshaanza kuyafanyia kazi mapungufu aliyoyaona katika mchezo wa kwanza dhidi ya Ihefu FC, ili kutorudia makosa.**

Sven alisema anatarajia mechi hiyo itakuwa na ushindani kutokana na wachezaji wa timu zote mbili kufahamiana vema na kila upande ukihitaji kuvuna pointi tatu muhimu.

"Kwenye mchezo wetu tuliocheza Mbeya, kikubwa kilikuwa kupata pointi tatu, tunashukuru tumezipata, lakini kama kocha nimeona yapo ambayo ni dosari kidogo ambazo nazifanyia kazi kabla ya mchezo wetu ujao," alisema Sven.

Kocha huyo alieleza mapungufu mengine aliyoyaona kwenye kikosi chake yalikuwa katika safu ya ulinzi na anaamini kuelekea mechi ya raundi ya pili yatakuwa yameondoka kabla ya kuingia uwanjani kuwakabili wapinzani wao hao.

"Kuna baadhi ya mapungufu kwenye safu yangu ya ulinzi, ninaamini yataondoka ndani ya muda mfupi na tutakuwa na mchezo mzuri siku ya Jumamosi," alisema Mbelgiji huyo.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema wachezaji wa timu hiyo wapo katika hali nzuri na baada ya kuwapa mapumziko ya siku moja, kikosi hicho cha mabingwa watetezi kitaanza rasmi programu ya mazoezi.

"Tunashukuru mchezo ulimalizika salama, hakuna majeruhi kwa sasa wachezaji wameelekeza mawazo na akili kwenye mchezo wetu unaofuata ambao tutacheza Morogoro dhidi ya Mtibwa Sugar," alisema Rweyemamu.

Aliongeza wamejipanga kukabiliana na changamoto katika mechi hiyo kwa sababu wanafahamu wenyeji wao ni moja ya timu zinazotoa upinzani kila wanapokutana.

"Tumejipanga na tunaamini wao (Mtibwa), pia wamejiandaa, tutaingia kwa kasi kwa sababu tunahitaji ushindi, ndio malengo yetu," Rweyemamu alisema.

Alieleza pia wachezaji wao watatu ambao ni Paschal Wawa, Luis Miquisson na Larry Bwalya waliokosekana katika mechi iliyopita wameshaungana na wenzao na wanaamini wataongeza nguvu katika kikosi hicho cha Wekundu wa Msimbazi.

Simba, ambao ni mabingwa watetezi walianza msimu mpya wakiwa ugenini kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu FC.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042